

DHIMA YA TASWIRA KATIKA NAHAU ZA KISAMBAA

NEEMA TANDIKO

**Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya
Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma**

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma na anapendekeza kuwa tasnifu inayoitwa *Dhima ya Taswira katika Nahau za Kisambaa* inafaa ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kama sehemu ya mahitaji kwa ajili ya tuzo ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Saini.....

Bi Zuhura Badru

(Msimamizi)

Tarehe

IKIRARI

Mimi, Neema Tandiko, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa, na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya aina yeyote.

Saini

Hairuhusiwi kuzalisha, kutafsiri, kunakiri, kupiga chapa, kuiga na wala kusambaza sehemu yeyote ya tasnifu hii kwa namna yeyote ile bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

SHUKRANI

Ninapenda kuwashukuru wote walionisaidia kwa namna moja ama nyingine hata kuihitimisha kazi hii. Ni vigumu kuwataja wote; hata hivyo, napenda kuwataja wachache. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uwezo wa kimwili, kiakili na nguvu za kuandika kazi hii.

Pili, ninapenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu Bi Zuhura Badru, kwa ushauri na mwongozo alionipa. Ameonesha ushirikiano mkubwa kwa kusoma sehemu mbalimbali za tasnifu hii, kukosoa, kutoa maelekezo na marekebisho na kuwa tayari kunihudumia pasipo kuchoka pale nilipohitaji msaada wake, pamoja na kuwa na majukumu mazito ya kitaaluma yanayohitaji uangalizi wake. Vilevile, napenda kuwashukuru wahadhiri wote walionifundisha ambao ni Prof Madumulla, Dkt S. Khatibu, Dkt M. Songoyi, pamoja na Dkt R. Sebonde kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha shahada yangu ya uzamili. Aidha, siwezi kumsahau mwalimu wangu Dkt A. S. Ponera kwa mwongozo na ushauri aliotoa katika maandalizi ya sehemu mbalimbali za tasnifu hii, kwani amekuwa na moyo wa kujitoa katika kukosoa na kunielekeza pale nilipohitaji msaada wake.

Tatu, Shukrani zangu ziuendee uongozi wa Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa (SEKOMU), wanafunzi wa shahada ya kwanza katika Fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu hiki, wazee waishio Soni, maktaba ya Mkoa wa Dodoma pamoja na Maktaba ya Taifa iliyopo jijini Dar es Salaam kwa ushirikiano walionipa katika utafiti huu.

Mwisho ni wazazi wangu Mzee Tumaini Tandiko na mama Miriamu Tumaini Tandiko, ninawashukuru kwa uzao wao, malezi yao, usimamizi wao, pia kunihimiza kuendelea kufanya kazi hii kwa moyo bila kukata tamaa, uwepo wao kwangu umekuwa msaada katika kipindi hiki chote cha maandalizi hadi kuikamilisha tasnifu.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa, uliongozwa na malengo matatu ambayo ni: kuchunguza namna taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa, kuchunguza athari zinazojitokeza katika matumizi ya taswira katika kufafanua na uelewekaji wa nahau za Kisambaa kwa hadhira pamoja na kutathimini uhusiano uliopo baina ya taswira zipatikanazo katika nahau za Kisambaa na maisha halisi ya jamii.

Mapengo yaliyojitokeza katika kutoa msukumo wa kufanya utafiti huu ni haya; Kwanza, wengi wa wataalam hao wamezishughulikia nahau kwa kuzikusanya na kuangalia maudhui yake kama walivyotajwa katika usuli wa tatizo la utafiti, hata hivyo, hawakukishughulikia kipengele cha taswira. Pili, uchunguzi wao umejigeza katika nahau za Kiswahili na lugha nyingine lakini sio lugha ya Kisambaa.

Mbinu ya udodosaji, mahojiano na mjadala wa vikundi zilitumika katika kukusanya data. Mbinu ya ufafanuzi ilitumika ambapo mkabala wa Umuundoleo ulitumika katika uchambuzi wa data. Vitongoji vitatu pamoja na Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa vilihusishwa katika kuwakilisha watafitiwa.

Matokeo ya utafiti yanabaini kuwa nahau za Kisambaa zimeenea katika vipengele mbalimbali vya maisha ya jamii hiyo. Nahau zilizochambuliwa zinaakisi mazingira yanayoihusu jamii hiyo pamoja na vitu vitumikavyo katika jamii husika.

Mchango mpya ambao umeibuliwa katika utafiti huu ni kukuza ufahamu juu ya matumizi ya taswira katika Fasihi, hususani katika kipengele cha fani ambapo taswira chomozi katika nahau za kisambaa zimeelezwa kama sehemu ya taaluma katika Fasihi simulizi ya Kiswahili.

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA KATIKA

UTAFITI

i. Nahau

Wamitila (2003) Anaeleza kuwa:

Nahau ni kama vikolezo vya kuutia utamu katika lugha inayohusika. Lugha zetu huwa na nahau au misemo mingi sana. Nahau huibuliwa kwa kiwango kikubwa katika lugha za kila siku kutokana na mahitaji na matumizi yake kwenye jamii. Baadhi ya nahau maarufu katika lugha ya Kiswahili zilianza kama misimu iliyokomaa kimatumizi na kuishia kukubalika na watumiaji wa lugha. Matumizi haya huvuka eneo la lile kundi dogo na kueleweka na jamii pana.

ii. Fani

Wamitila (2008) naye anaeleza kuwa:

Fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia lugha, pia fani ni ufundi au ustadi autumiao msanii katika kuijenga kazi yake. Lugha hiyo huwa na sifa fulani, kwa mfano ina vikolezo au vitia radha fulani, imesheheni au kujaza mbinu za kila aina. Haiwezekani kwa mwandishi kuisawilisha dhamira yake bila ya kuitegemea fani. Ikiwa mwandishi atataka kuwasiliana na msomaji wake vyema pamoja na hata kumshawishi na kumwathiri ipasavyo lazima aitumie lugha yake vyema au ahakikishe kuwa lugha yake ina uwezo wa kuuwasilisha ujumbe huo. Uhusiano wa fani na maudhui ni muhimu sana na hutegemeana, moja ni kama upande mmoja wa sarafu.

iii. Taswira

Senkoro (2011) anafasili dhana ya taswira kuwa:

Ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi za Fasihi. Anaendelea kufafanua kuwa mara nyingi taswira huambatana na matumizi ya tamathali za semi hasa za sitiari na tashibiha.

iv. Semi

Simiyu (2011) Anasema kuwa:

Semi ni fungu la maneno ambalo huwa fupi linalotumia ishara, picha na tamathali za semi kwa ufundi wa hali ya juu. Ameendelea kusema kuwa, matumizi ya tungo fupi zenye ishara na picha huziwezesha kukumbukwa kwa urahisi.

v. Nadharia

Wamitila (2003:393) Anaeleza kuwa “nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kueleza hali fulani, chanzo chake, muundo wake, utendaji kazi wake na mwingiliano wake wa ndani na nje”.

YALIYOMO

ITHIBATI	i
IKIRARI.....	ii
SHUKRANI.....	iii
IKISIRI.....	iv
UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFIGI.....	v
YALIYOMO	vii
ORODHA YA PICHA.....	x
ORODHA YA VIFUPISHO	xi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti	3
1.3 Malengo ya Utafiti	4
1.3.1 Lengo la Jumla	4
1.3.2 Malengo Mahususi	4
1.4 Maswali ya Utafiti.....	4
1.5 Umuhimu wa Utafiti	4
1.6 Mipaka ya Utafiti	5
1.7 Nadharia ya Uchambuzi wa Data za Utafiti.....	5

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO.....

2.1 Utangulizi.....	8
2.2 Mapitio Kuhusu Semi katika Kazi ya Fasihi	8
2.3 Mapitio Kuhusu Taswira kwa Ujumla	20
2.3.1 Matumizi ya Taswira	21
2.3.2 Aina za Taswira	21
2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko	23
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili	24

SURA YA TATU: USANIFU WA MBINU NA VIFAA VYA UTAFIGI

3.0 Utangulizi.....	25
3.1 Mpango wa Utafiti	25

3.2 Jamii ya Watafitiwa	26
3.2.1 Walengwa wa Utafiti	26
3.2.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji wake	26
3.3 Ukusanyaji wa Data	27
3.3.1 Zana za Kukusanyia Data	28
3.3.2 Njia ya Kukusanyia Data	28
3.3.2.1 Dodoso	28
3.3.2.2 Mahojiano	29
3.3.2.3 Mjadala wa Vikundi	29
3.3.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti wake	29
3.3.4 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti	30
3.4 Uchanganuzi wa Data	31
3.5 Muhtasari wa Sura ya Tatu	31

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA

UTAFITI	32
4.1 Utangulizi	32
4.2 Taswira Zinavyojitokeza katika Nahau za Kisambaa	32
4.2.1 Taswira za Kuonekana	33
4.2.2 Taswira za Kufikirika	37
4.3 Athari ya Taswira katika Nahau za Kisambaa katika Ufafanuzi na Uelewekaji Wake kwa Hadhira	39
4.3.1 Athari Chanya	39
4.3.1.1 Taswira Humwezesha Hadhira Kupata Undani wa Nahau	40
4.3.1.2 Taswira Hutusaidia Kuweka Kumbukumbu ya Kudumu Akilini mwa Msomaji ama Msikilizaji	44
4.3.1.3 Taswira Itumikapo katika Neno Humjengea Hadhira Udadisi	46
4.3.2 Athari Hasi	49
4.3.2.1 Kuleta Utata katika Matumizi yake Kulingana na Mfanano wake Kimaana	49
4.4 Uhusiano uliopo Baina ya Taswira Zilizomo Ndani ya Nahau za Kisambaa na Uhalisi wa Maisha ya Jamii	53
4.4.1 Huakisi Maisha Halisi katika Jamii Husika	54
4.4.2 Muhtasari wa Sura ya Nne	59

SURA YA TANO: MHUTASARI, HITIMISHO, MAPENDEKEZO.....	60
5.1 Utangulizi.....	60
5.2 Mhutasari wa Tasnifu.....	60
5.3 Utoشهlevu wa Nadharia Iliyotumika katika Utafiti	61
5.4 Mchango Mpya wa Utafiti Huu	61
5.5 Mapendekezo Juu ya Tafari Zijazo.....	63
MAREJELEO	64
VIAMBATISHO	66

ORODHA YA PICHA

- Picha namba 1: Mtafiti (aliyevaa sweta jeupe) akiwa na wanachuo wa shahada ya kwanza ya Fasihi simulizi wakiwa katika mjadala wa vikundi. (Utafiti, Juni, 2015).....78
- Picha namba 2: Mtafiti (upande wa kulia) akiwa katika vikundi vya watafitiwa na kutoa msaaada kwa watafitiwa pale inapobidi, (Utafiti, Juni, 2015)78
- Picha namba 3: Mtafiti (upande wa kulia) akiwa na watafitiwa katika kujadili uhusiano uliopo kati ya matumizi taswira katika nahau za Kisambaa na maisha halisi katika jamii, (Utafiti, Juni, 2015)79
- Picha namba 4: Mtafiti (upande wa kushoto) akiwa na watafitiwa wakitoa michango yao kuhusu athari zinazojitokeza katika matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa (Utafiti, Juni 2015).....79
- Picha namba 5: Mtafiti akiwa katikati akinukuu michango ya wazee kuhusu athari wazipatazo ndani ya nahau katika nahau za Kisambaa, (Utafiti, Juni, 2015)80

ORODHA YA VIFUPISHO

Bi	Bibi
Dkt	Daktari
DUP	Dar es Salaam University Press
EAEP	East Africa Educational Publishers
EPD	Educational Publisher Distribuers
OUP	Oxford University Press
Prof	Profesa
SEKOMU	Sebastian Kolowa Memorial University
TPH	Tanzania Publishing Housing
TUKI	Taasisi ya Uchambuzi wa Kiswahili
UDOM	University of Dodoma

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Sura hii inatambulisha usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, manufaa ya utafiti, nadharia ya utafiti pamoja na mipaka ya utafiti.

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Dhana ya nahau imefafanuliwa na kujadiliwa na wataalam mbalimbali katika Fasihi. Mulokozi (1989:35) anaeleza kuwa: “nahau ni misemo ya picha ambayo huleta maana iliyofichwa, ni lugha yenye uzito zaidi kuliko semi za Kiswahili au lugha ya kawaida ya moja kwa moja” Pia, Mulokozi aliendelea kufafanua kuwa: “nahau ni semi zenye undani, undani ambao wageni wanaoijua lugha hiyo juu juu tu huambulia patupu wanapoambiwa nahau hizo, kwani nahau licha ya kuwa lugha ya mkato, lakini, ina ujumbe mzito wa mafumbo”.

Wamitila (2003:264) naye anasema kuwa: “Nahau hutumiwa kuelezea aghalabu, kitenzi, jina na kauli zilizoundwa kwa lugha ya kawaida lakini zenye maana iliyofichika au isiyokuwa ya kawaida”.

Kutokana na maelezo hayo ya Mulokozi na Wamitila tunaweza kusema kuwa, nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi.

Wataalam mbalimbali wameeleza kuwa asili na chanzo cha nahau hutokana na mazingira halisi na shughuli za kijamii za kila siku. Kuhanga (1976:97) ameeleza kuwa: “Mtu anaweza akapatwa na jambo fulani na hapo hapo hilitungia nahau kama onyo, ama fundisho kwake, na kwa jamii yote, pia, kumliwaza kwa yale yote yaliyomtokea”.

Hivyo, tunaweza kusema kuwa, katika lugha yoyote ile neno huwa na mazingira yake ambayo husaidia kuifafanua maana ya neno hilo kwa wazi zaidi, wakati mwingine tunalikuta neno fulani limezungukwa na mazingira maalumu, huku maana yake ikitegemea juu ya mazingira hayo tu na sio mengine.

Kuwepo kwa hali ya watafiti mbalimbali kutopenda kufanya tafiti katika lugha za kibantu hasa kushughulikia kipengele cha nahau, kumefanya lugha za kibantu kutojulikana vizuri hasa nahau za Kisambaa. Pia, kwa jamii nyingine kumezifanya zisifahamike katika upana wa matumizi yake. Vilevile, maelezo haya yanatoa mwanga wa kuweza kuchunguza jinsi nahau zinavyotumia taswira katika uga wa Fasihi simulizi, kwani mara nyingi waandishi wamekuwa wakilitazama suala la matumizi ya taswira katika kazi za Fasihi andishi kwa upana. Mifano ya watafiti mbalimbali waliotafiti kazi za kifasihi katika taswira ni pamoja na Nyenye (2011) ambaye ameshughulikia kipengele cha taswira zinazojitokeza katika nathali za Kezilahabi; Masungwa (2012) aliyechambua taswira na ishara katika ushairi wa Mnyapara, pamoja na Mrekwa (2013) aliyechambua taswira katika ushairi wa Kaluta.

Taswira ni miongoni mwa vipengele vya lugha katika kazi za Fasihi, ambapo hubeba dhima ya kuchota hisia za msikilizaji au msomaji na kumfikisha katika kuyatambua maudhui ya kazi hiyo kwa kumuundia picha na ishara mbalimbali. Dhana ya taswira kwa muktadha wa Fasihi hufafanuliwa kama istilahi inayoambatana na matumizi ya tamathali za semi, hasa sitiari na tashibiha.

Kamusi ya Kiswahili Karne ya 21 (2011) imeeleza kuwa:

Jazanda ni sawa na picha ya kitu iliyomo kichwani mwa mtu. Kwa mujibu wa kamusi hiyo jazanda ni sawa na taswira. Taswira hunasa hisia za wasomaji na wasikilizaji wa kazi ya Fasihi kwa kuumba picha ya kitu akilini mwa mtu. Matumizi ya picha kwa asilimia kubwa huambatana na tamathali za usemi ambazo ni vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zisizofanana. Miongoni mwa tamathali za usemi ni sitiari inayofananisha vitu viwili au zaidi bila viunganishi. Nyingine ni tashibiha inayolinganisha vitu kwa kutumia viunganishi, maneno kama vile; kama kwamba, mfano wa, mithili ya na maneno mengineyo.

Hivyo, ufafanuzi huu umeweza kutoa mwanga kwa mtafiti wa kuweza kuchambua na kuchunguza matumizi ya taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa, kwa kuzingatia muktadha ili kuweza kuona ni kwa namna gani lugha ya taswira hutumiwa kujenga picha akilini mwa msomaji au msikilizaji katika kazi ya Fasihi.

1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wataalamu mbalimbali wamefanya utafiti kuhusu nahau za Kiswahili pamoja na zile za lugha nyingine, wameshughulikia zaidi kipengele cha maudhui na baadhi ya vipengele vya fani ambao ni Senkoro (1982) alizikusanya nahau za Kiswahili na kuchunguza maudhui, muundo pamoja na mtindo wake, Madumula (1995) alichunguza nahau na misemo katika jamii ya Wahehe, naye Wamitila (2003) alichunguza maudhui ya nahau za Kiswahili. Hata hivyo, hawakushughulikia kipengele cha taswira katika nahau za Kisambaa, hawakukishughulikia kipengele cha taswira kwasababu wao walijikita katika maudhui zaidi, jambo ambalo limetoa msukumo mtafiti kufanya utafiti juu ya matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa. Utafiti huu ulilenga kuchunguza kipengele cha taswira katika nahau za Kisambaa.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa.

1.3.2 Malengo Mahususi

- a) Kuchunguza namna taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa;
- b) Kuchunguza athari ya taswira katika ufafanuzi na uelewekaji wa nahau za Kisambaa kwa hadhira,
- c) Kutathmini uhusiano uliopo baina ya taswira zilizomo kwenye nahau na maisha halisi ya jamii.

1.4 Maswali ya Utafiti

- a) Ni kwa namna gani taswira zinajitokeza katika nahau za Kisambaa?
- b) Matumizi ya taswira yanaathiri vipi ufafanuzi na uelewekaji wa nahau za Kisambaa kwa hadhira?
- c) Kuna uhusiano gani kati ya taswira zilizomo kwenye nahau na maisha halisi ya jamii?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuleta tija zifuatazo; Kwanza, Kukuza ufahamu juu ya matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa ikiwa ni sehemu ya taaluma katika Fasihi simulizi. Pili, kuongeza ufahamu kuhusu matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa na uhusiano wake na maudhui yabebwayo na nahau hizo. Tatu, kupitia nahau za Kisambaa, jamii itaweza kutofautisha nahau na vipengele vingine vya

Fasihi simulizi katika semi kama vile misemo, vitendawili na methali. Vilevile matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumika kama sehemu ya marejeleo katika kazi ya Fasihi.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa ambazo zilionekana kusheheni matumizi ya taswira. Pia ulizingatia malengo mahususi yaliyokusudiwa katika utafiti huu, vilevile kazi mbalimbali za Fasihi simulizi zilitumika katika mawanda haya ya utafiti.

1.7 Nadharia ya Uchambuzi wa Data za Utafiti

Utafiti huu ulitumia nadharia ya Umuundoleo. Kwa hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake umefanywa kwa kuzingatia nguzo ya nadharia hii.

Umuundoleo ni nadharia iliyoibuka kutokana na mawazo yanayohusishwa na isimu-muundo ambayo kitovu chake ni Ferdinand De Saussure katika miaka ya arobaini. Nadharia hii inapinga mawazo yaliyomo katika nadharia ya Umuundo ya kuzikita ishara katika mfumo wa lugha ambao wanauona kuwa ni funge, kwa Wana-Umuundoleo maana ya ishara hubadilika kulingana na miktadha tofauti. Mikabala mingine ya kiuhakiki yenye ukaribu sana na mkabala huu ni nadharia ya Semiotiki na nadharia ya mwitik (i) o wa msomaji. Nadharia hizi zote zinaona kuwa kazi ya Fasihi huwa na uwazi fulani unaoweza maana nyingi na mbalimbali kutolewa kuhusu kazi hiyo moja. Aidha, nadharia hizi hushughulika na kuwachunguza wasomaji wanavyoitikia kazi za kifasihi.

Nadharia hii inahusishwa zaidi na mhakiki wa kifaransa Jacques Derrida na wengine kama Julia kristeva, Michael Foucault, Jacques Lacan na Louis Althusser.

Misingi ya nadharia hii ni kuwa;

i/ Lugha inachukua nafasi kubwa katika kuuhakiki na kuuchanganua muundo wa kijamii wa maana pamoja na uwezo wa ung'amuzi au urazini wa binafsi.

Hivyo, maana ya lugha huundwa kutokana na mazoezi ya kiusemi yaani kijamii, kisiasa na kiuchumi.

ii/ Umuundoleo unaangalia lugha kama nguzo ambapo maana halisi au inayowezekana huelezwa.

iii/ Kwa wana Umuundoleo maana ya ishara hubadilika kulingana na miktadha tofauti.

Dhana ya 'uhusikanafsi' hii huundwa kwa matumizi ya lugha kwa mantiki kwamba, maana ya lugha huundwa kutokana na mazoezi ya kiusemi yaani kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa msingi huu lugha huakisi na kuonyesha hali halisi ya kijamii pamoja na kuutungia uhalisi. Hivyo, dhana hii ilisaidia katika kuhusisha taswira zitumikazo katika nahau za Kisambaa na hali halisi ya maisha katika jamii husika kwa kuzingatia maana halisi au zinazowezekana.

Wana-Umuundoleo wanasisitiza kuwa maana ya lugha hukitwa kwenye muktadha wa kiusemi au wa kimazungumzo, hivyo, huweza kubadilika kutegemea muktadha wa kiusemaji. Hivyo basi, mawazo haya yamesaidia katika kuzihusisha taswira katika nahau za Kisambaa katika miktadha mbalimbali kulingana na maana zilizopatikana. Wana - Umuundoleo wanaeleza kuwa, kwa kawaida ishara huwa na maana nyingi, hii ni kwa sababu maana hujengwa na lugha, na lugha anayoipata mtu huwa ni matokeo ya maingiliano ya kijamii, ambayo huwahusisha wazungumzaji

binafsi, na hivyo maana au kiashiriwa hakiwezi kuwa funge, kutokana na hoja hii ni wazi kuwa hadhira katika kazi ya Fasihi si mpokeaji tu bali na msanii pia, kwani hushiriki kuipa maana kazi husika.

Kahigi na Mulokozi (1982) juu ya dhana hii wamefafanua kuwa:

Msomaji wa matini hupata maana anapozinduliwa na ustadi wa mshairi wa matumizi ya lugha, hivyo, huhusisha kile kilichoumbwa na msanii na hali halisi anayojua. Kwa maana hiyo, uhusishwaji huu husaidia kuibua maana ya kazi ya kifasihi na kuelewa umuhimu wake.

Sasa basi, tunaweza kusema kuwa nadharia ni mwongozo unaomwelekeza mpokezi wa kazi ya Fasihi kuifahamu kazi ya Fasihi kwa undani zaidi. Nadharia inaweza kuundwa kutokana na tajiriba ya mtu binafsi au juhudi za kikundi cha watu. Vilevile nadharia ni kama dira inayowapa wapokezi vigezo sawa vya kuzithamini kazi za Fasihi.

Jinsi nadharia hii ya Umuundoleo ilivyotusaidia katika utafiti huu ni kwamba; kwanza, dhana hii imetupeleka katika haja ya kutambua na kuelewa jinsi taswira zinaavyotumika katika nahau kadhaa za Kisambaa tulizozipata. Pili, tumeweza kufahamu kuwa maana ya lugha huundwa kutokana na mazoezi ya kiusemi yaani kijamii, kisiasa na kiuchumi, kwani lugha huakisi na kuonesha hali halisi ya kijamii pamoja na kuutungia uhalisi. Tatu, dhana hii ilitusaidia katika kuhusisha taswira zitumikazo katika nahau za Kisambaa na hali halisi ya maisha katika jamii kwa kuzingatia maana halisi au zinazowezezana, vilevile tumepata kufahamu kuwa maana ya kiashiriwa haiwezi kuwa funge ila hutegemea mazingira lilipotumika na kumpatia hadhira maana. Hivyo, ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishwaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia hii ambao ni lugha katika viwango mbalimbali, ambapo ilimsaidia mtafiti kuchanganua mambo ya kiishara na taswira ambazo zimeweza kuchomoza ndani ya nahau za Kisambaa.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada hii. Machapisho hayo yamegawanywa katika makundi makuu mawili; la kwanza lilihusiana na maandiko yaliyogusia semi. Pili ni maandiko kuhusu taswira katika Fasihi kwa jumla.

2.2 Mapitio Kuhusu Semi katika Kazi ya Fasihi

Mara nyingi semi hutumia lugha ya picha na ishara ambayo hujitofautisha na lugha nyingine za kawaida. Semi husaidia kuongeza radha ya mazungumzo ya kawaida, mashairi na hadithi, vilevile Semi hutumika katika jamii tofauti. Aidha Semi hutumika katika sehemu mbalimbali ambazo ni rasmi na hata ambazo si rasmi kwa kutoa ushauri au nasaha. Wachambuzi wengi wamejaribu kuzichambua semi kwa mitazamo tofauti, na zimechambuliwa kwa kuangalia vipengele vya fani na maudhui yake kwa jumla.

Balisidiya (1987:2-9) amefafanua semi kuwa “ni fungu la tungo za Fasihi simulizi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Ni mafumbo yanayokusudiwa kubeba maudhui yenye maana zinazofuatana na ibara mbalimbali za matumizi ya taswira”. Balisidiya ameugawa utanzu wa semi katika tanzu zifuatazo: methali, vitendawili na misemo.

Hivyo, kutokana na maelezo hayo ya Balisidiya ni dhahiri kuwa kipengele cha semi ni muhimu katika kazi ya kifasihi, hususani katika Fasihi simulizi, na hii ilimsaidia mtafiti kuweza kukichunguza kipengele cha nahau za Kisambaa kama sehemu ya

semi ili kuweza kuona matumizi ya ishara na picha jinsi zinavyojitokeza katika nahau hizo.

Mulokozi (1990) naye anafafanua kuwa:

semi ni tungo au kauli fupi fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo muhimu ya kijamii. Kumbo hili linazo tanzu zifuatazo; methali, vitendawili, simo (misimu), mafumbo, lakabu na kauli tauria.

Katika andiko hili tunapata mkanganyiko kuwa Mulokozi hakuweka wazi kuwa ni kiwango gani cha ufupi wa tungo anachokizungumzia kwani hata kazi nyingine za kifasihi zinaweza kufupishwa kwa nahau, pia nahau zaweza kuvyaza kazi za kisanaa, hivyo, tunaona kuwa nahau na kazi nyingine za kisanaa ni vitu vinavyotegemeana katika kazi za kifasihi . Na kupitia maelezo haya mtafiti amepata fulsa ya kuzichunguza nahau hizo ili kuweza kupata zaidi yaliyomo katika kipera hiki cha semi.

Mauya (2006:38) naye anazifafanua semi kuwa, “semi hutumika katika maisha ya kila siku kwa kupitia masimulizi mafupi. Dhamira ya masimulizi hayo ni kuelimisha na kuburudisha”. Amezigawa semi katika nahau, misemo na methali. Hivyo, mtafiti aliona kuwa maelezo hayo yametoa mwanga kwa mtafiti, kuwa semi ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya jamii katika uhalisi wake.

Wamitila (2004) naye anaeleza kuwa:

Nahau ni vifungu ambavyo hutumiwa kwa maana fulani ambayo huenda isiafikiane na maana halisi ya maneno yanayohusishwa kwenye vifungu hivyo huwa na muundo fulani na aghalabu usiobadilika japo maana zenyewe huweza kubadilika au kupambanuliwa. Nahau hutumika kuelezea kauli zilizoundwa kwa lugha ya kawaida lakini zenye maana iliyofichika au isiyokuwa ya kawaida.

Katika andiko hili tumefahamu kuwa maana katika nahau hutegemea muktadha jinsi neno hilo lilivyotumika. Kutokana na ufafanuzi huo mtafiti alipata hamasa ya

kuchunguza nahau za Kisambaa, ili kuona ni kwa namna gani nahau zinavyotumika kulingana na muktadha, na kwa jinsi gani nahau hizo zinavyoweza kuathiri hadhira wake katika kupata maana.

Douglas Biber na wenzake (2002:9-48) anasema kuwa “nahau hutofautiana kiuwazi, hata maana zake zinatokana na maana ya maneno ya kawaida zipo zenye kutumia maneno rahisi, na pia, zipo zenye kutumia maneno magumu”. Pia andiko hili limetufunza kupambanua matumiza mbalimbali ya nahau kwamba, zipo zinazotumia maneno ya kawaida na pia zitumiazo maneno ya kiufundi, zikiwa na dhumuni la kumfikirisha hadhira katika kulifahamu kusudio la fanani.

Senkoro (1982) anasema kuwa:

Nahau hutumiwa kutambulisha mazingira maalum au kuijulisha hadhira wakati unauhusika katika kazi ya Fasihi inayoshughulikiwa, vilevile, nahau hutumika kwa lengo la kupamba kazi ya Fasihi na pia kuwaainisha wahusika na lugha zao. Pia, nahau ni msemu unaojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida, lakini, ambayo huwa yamesetiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno hayo katika matumizi ya kawaida.

Vilevile, katika ufafanuzi wa Senkoro tunapata kufahamu kwamba nahau hutambulisha mazingira ya matumizi ya nahau, pia, andiko hili lilimsaidia mtafiti katika kazi yake kuchunguza namna nahau za Kisambaa zinavyotumika katika muktadha maalum na kuweza kuwaainisha wahusika hao pamoja na jamii yake.

Vilevile, Senkoro amezigawa sifa bainifu za nahau kama ifuatavyo;

A/. Nahau kuwa sawa na neno kimaana.

Likiwa ni fungu la maneno wakati huo huo ni sawa na neno moja kimaana, yaani maana yake haijumuishi kutokana na maana ya neno moja lililomo ndani ya fungu

hilo. Jambo lenye kuthibitisha hayo ni kwamba neno moja kwa kufichua wazo halisi la nahau hii au nyingine, mifano ya nahau hizo ni:

- (i) Kupata jiko - kuo
- (ii) Kuangusha uso - kutahayari
- (iii) Kushika hatamu - kuongoza

Nahau nyingine hata zinakaribiana huwa neno moja kwa umbo lake badala ya fungu la maneno na aghalabu huandikwa kama neno moja.

Mfano: (i) Dondandugu - jambo lisiloweza kugangika

- (ii) Kidudumtu - mfitini
- (iii) Ndumakuwili – mnafiki

Jambo jingine lenye kuthibitisha sifa za kineno za nahau ni uwezo wa nahau kama ilivyo kwa maneno mengine kuwiana miongoni mwao kwa njia zifuatazo;

Nahau zenye mfanano wa maana lakini zilizoundwa kutokana na maneno tofauti

Mfano: (i) Kuona cha mtema kuni

- (ii) Kuona kilichomtoa kanga manyoya

Nahau zote hizi zina maana ya kuona jambo la hatari au kisasi kutokana na ubaya ulioufanya.

Mfano (i) Pata jiko

- (ii) Kuasi ukapera

Nahau zote hizi mbili pia zina maana sawa yaani kuo.

- (i) Kula mwande
- (ii) Kwenda mrisi

Pia nahau hizi mbili zina maana ya kukosa ulichokitumainia

Nahau zilizo na maana ya kinyume lakini zenye umbo la sawasawa isipokuwa neno moja (umbo husababisha kinyume hicho)

Mfano: (i) Kula unga - kupata kazi

(ii) Kumwaga unga - kuachishwa kazi

(c). Nahau zenye mfanano wa umbo na muundo lakini zilizo na maana mbalimbali;-

Mfano; (i) Kuzunguka mbuyu - kutoa rushwa

(ii) Kwenda kinyume - kudanganya

(iii) Kunywa maji - kuishi kwa dhiki

(iv) Kushika miguu- kutoa shukrani, kupiga mbio, kuomba radhi

B/. Nahau kuwa na maana ya kisarufi

Nahau hutumika katika sentensi na uwiano wake pamoja na maneno mengine ndani ya sentensi hiyo huwa ni ule ule kama ulivyo baina ya neno moja na maneno mengine, yaani nahau inaweza kupatana na neno jingine kwa kuchukua ngeli, wingi au wakati wake, kutegemea juu ya neno jingine au kujumuika nalo, mfano Mfalme alipoona ya kuwa watu wote wamekuwa kinyume na kimya kingi kina mshindo akang'amua mara moja kuwa *ushawishi_wa waziri mkuu haukufua dafu*, mabepari *wanaipikia majungu Afrika_huru*, mazungumzo yao yalikuwa ya *ana kwa ana*. Kutokana na sifa zilizotajwa, yaani nahau kuwa na maana ya kisarufi, nahau huweza kulinganishwa na kitenzi, jina, kivumishi na kielezi kuzigawa. Nahau za Kiswahili tungeweza kuzigawanya katika makundi manne ya kimsingi.

a/. Nahau – majina

Mfano: - (i) Joka la mdimu

(ii) Ndege mbaya

b/. Nahau - vitenzi

Mfano: (i) kukaanga mbuyu

(ii) Kufua dafu

c/. Nahau - vivumishi

Mfano: (i) Si hayati si mamati

(ii) Kifupi nyundo

d/. Nahau - vitenzi

Mfano: (i) Kufa kupona

(ii) Kufumba na kufumbua

Katika sentensi kama tulivyokwisha kusema nahau huchukua maana ya neno moja na kuhusiana na mengine kama neno moja, kwa hiyo ni sawa na jina au kitenzi ambavyo vinaweza kuchukua ujumbe wa nafsi kitendwa, kibainishi, kielezi na kiarifu, nahau pia inaweza ikachukua majukumu mbalimbali katika sentensi.

Mfano (katika sentesi zifuatazo, maneno yaliyoandikwa kwa hati mlazo ni nahau ambazo zimetumiwa na wasemaji ili kuweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa);

Mimi *langu jicho*, hapa neno lililoandikwa kwa hati mlazo ni kiarifu.

Baada ya kupata *kifungua kinywa*, hapa neno lililoandikwa kwa hati mlazo ni kitendwa

Walipigana *kufa kupona*, neno lililoandikwa kwa hati mlazo ni kielezi cha namna.

Kwa mapendo aliyokuwa nayo juu ya mwanawe ikawa kila siku *kiguu na njia* kwa tabibu lililoandikwa kwa hati mlazo ni kielezi.

C/. Nahau na umbo lako

Sifa nyingine muhimu ya kutambulisha nahau ni nahau kuwa fungu la maneno zaidi ya neno moja na lenye umbo na muundo maalumu. Lakini kutokana na sifa tulizokwisha kuzichambua haiwezekani kudai kwamba nahau ni sawa na fungu la maneno la kawaida. Kila fungu la maneno ambalo si nahau ni majumuisho ya maneno yenye kudumisha au kubakiza sifa na maana zake za kineno, ilihali nahau hujumuisha maneno yaliyopoteza sifa na maana zake za kawaida na kuchukuliwa kimaana kama neno moja. Nahau na fungu moja la maneno huwa na uwiano wa kiasili tu, yaani kama kawaida kwa kuchukua maana yake asilia na kuipanua kwa kuongeza maana maalum ya mafumbo. Katika lugha ya kisasa nahau nyingine zimepatikana sambamba na mafungu ya maneno yaliyokuwa chanzo cha nahau hizo,

Mfano: - kutonesha kidonda kuzunguka mbuyu

Lakini tukiitumia mifano hiyo katika sentensi tutaona kwamba nahau haiwezi kusawazishwa na mafumbo ya maneno ya kawaida, tofauti yake iko katika maana iliyokusudiwa.

(i) Ulipozungumzia juu ya maradhi ya kifua kikuu, aliondoka, huku machozi yakimlengalenga kwani *ulitonesha kidonda* cha kufiwa na baba yake kwa maradhi kama hayo hayo.

(ii) Ni bora mngoju huyo alazwe hospitalini kwani akiwa nyumbani haachi *kutonesha kidonda chake*.

Nahau “kutonesha kidonda” katika mfumo wa kwanza inafahamika kama kauli moja ambayo kimaana ni mbali na neno “kutonesha” au “kidonda”. Maana yake ni kukumbusha msiba uliokwishapita na kusahauliwa, katika mfano wa pili maana ya fungu la maneno hilo hilo inafahamika kutokana na kila neno “kutonesha” na neno “kidonda”.

Hali kadharika tofauti baina ya nahau na fungu la maneno imo katika umbo lake. Ili kuelewa tofauti hiyo hebu tuchunguze sifa za umbo la nahau kwa undani.

D/ Sifa za Umbo la Nahau

a/. Idadi ya maneno yenye kuunda nahau

Kama tulivyokwisha kusema nahau ni lazima hujumuisha maneno si chini ya mawili. Lakini idadi yake inaweza kuwa zaidi ya mawili. Tukiitambua barabara idadi ya maneno ya nahau tunaweza kuipambanua nahau hiyo ndani ya sentensi kwa urahisi zaidi.

Mfano:- Hakupenda kwenda alikoambiwa lakini alikubali *shingo upande*, Neno “alikwenda” liko karibu sana na kuhusiana moja kwa moja na nahau “shingo upande” ambayo ina maana ya “bila kupenda” na ujumbe wa kielezi katika sentensi. Lakini neno hilo haliingii katika nahau yenyewe kwa sababu limebakiza maana yake asilia na ujumbe wake kama kiarifu katika sentensi.

ii /. Mipaka ya nahau

Ili kuelewa barabara umbo la nahau na uwiano wake pamoja na maneno mengine ya sentensi, hatuna budi kutambua idadi ya maneno yenye kuiunda nahau, na mipaka yake pia. Maneno mengine yanaweza kuingia katika mipaka ya nahau na kuhusiana

na nahau hiyo kutokana na ujumbe wake katika sentensi, lakini maneno hayo hayaingii ndani ya nahau yenyewe.

Nao waganga wakazua uongo kwa *kutia chunvi* nyingi wakati wakitangaza hayo maajabu ambayo yanaweza kutendwa na mkia wa jitu.

Neno “nyingi” linatilia nguvu tu nahau “kutia chumvi” na limo katika mipaka yake, haliingii katika nahau

Mzee huyu *amekula chunvi nyingi*, hapa neno “nyingi” linaingia moja kwa moja katika nahau.

iii/. Kutofautika kwa umbo la Nahau.

Viungo vya nahau nyingine huwa vina maumbo tofauti, tofauti hizo zinaweza kudhihirika katika mielekeo miwili, yaani mwelekeo wa kimofolojia na ule wa kimaneno.

Mfano: -‘kazi ya “kijungu jiko” au “kijungu meko”, “kuuma kidole”, “ kuwa na mkono mrefu”.

Hizi tofauti za kimofolojia

“kukata jongoo kwa meno” au “kuuma jongoo kwa meno” Kuondoa mbeleko” au “kuvunja mbeleko” “kupanda shetani” au “kupanda ibilisi”. Hizi ni tofauti za maneno kama tulivyoona mabadiliko yaweza kuhusu kiungo kimojawapo tu au viungo vyote vilivyomo ndani ya nahau.

iv/. Ukamilifu wa umbo la nahau

Katika sentensi nahau nyingine zinaweza kutumika na umbo lake kamili au lisilo kamili.

Mfano mwalimu alipojaribu kumweleza baba mtoto kisa cha kumwadhibu mwanawe kwa fimbo, mzazi *akaja juu kwa maneno*. “Maneno haya ya nini” Tim alitia tambara kinywani mwa baba yake ambaye alianza *kuja juu* kwa kuona pesa na ugumu wa roho, ya mangi, katika sentensi hizo mbili kumetumiwa nahau ile ile moja yenye maana “kukasirika au kughadhibika” lakini katika mfano wa pili nahau hiyo haikutiwa na umbo lake kamili.

Sifa ya tatu na ya nne yaani kutofautika kwa umbo la nahau na ukamilifu wa nahau ni muhimu hasa kwa ajili ya kutofautisha nahau na mafungu ya maneno ya kawaida. Nahau ilibadiliwa au kuondoshewa neno fulani, hubakia kuwa na maana ile ile ilhali kuongezwa, kubadilishwa au kuondoshwa maneno katika mafungu ya kawaida hakukosi kuleta maana nyingine.

Mtu yule tuliyemkuta sokoni na huyu aliyepita sasa hivi, ni *reale kwa ya pili*, nadhani hawa ni ndugu.

Hapo tunaweza kubadilisha neno “reale” kwa neno “rupia” bila ya kuikadilia maana ya nahau yaani “mfano mmoja au sawasawa”, katika mkusanyiko wake wa sarafu anazo *rupia mbili* na reale moja. Hapa kila fungu la maneno huleta maana yake mbalimbali.

v /. Mitindo ya muundo wa Nahau

Nahau za Kiswahili zinaweza kuundwa kwa mitindo mbalimbali. Mitindo iliyo maarufu zaidi ni kama hii ifuatayo

a/. Kitenzi + jina

Mfano:(i) Kuvunja mbeleko

(ii) Kuwa macho

b/ Kitenzi +jina + vielezi au vivumishi

Mfano: (i) Kuwa na mkono mrefu

(ii) Kuficha jua kwa ungo

c / Kitenzi + Ktenzi

Mfano: (i) Kufa kupona

(ii) Kufumba na kufumbua

d / Kitenzi + Kielezi

Mfano: (i) Kufa kiofisi

(ii) Kufa kingoto

e / Jina + Kitenzi

Mfano: (i) Akili kumruka (mtu)

(ii) Miguu haimshiki (mtu)

f /. Jina +Jina

Mfano: (i) Donda ndugu

(ii) Domo kaya

g / Jina + kiunganishi+ Jina

Mfano: (i) Ana kwa ana

(ii) Bega kwa bega

h / Jina+ Kivumishi

Mfano: (i) Chungu nzima

(ii) Bahari kubwa

i / Neno saidizi + Jina

Mfano: (i) Hata chembe

(ii) Kwa mikono miwili

j / Nahau zenye muundo wa sentensi

Mfano: (i) Si hayati si mamati

(ii) Kisu kimepata mfupa

(iii) Wewe kisu mimi nyama

Tumekwisha kuona kwamba takribani nahau zote zimeundwa kwa mitindo sawa na ile ya mafungu ya maneno na hata sentensi zilizokuwa chanzo au asili ya nahau zinazohusika. Lakini mfanano huo wa mitindo ni wa kijuu juu tu, kumbe muundo wa nahau una umuhimu wa kindani zaidi katika kuelewa sifa za nahau, kwa hivyo inafaa hapa kuchambua namna gani muundo wa nahau unavyolingana na sifa zake za kimaana na kisarufi, yaani kuhusika kwake na kundi hili au jingine la nahau, kama vile nahau –majina, nahau-vitenzi.

Hii pia imetoa hamasa kwa mtafiti kuchunguza nahau za Kisambaa ili kuweza kutambua ni nahau zipi katika nahau za Kisambaa zitumiazo maneno ya kawaida na zile zinazotumia maneno magumu.

E/ Dhima ya Nahau

Nahau, kama zilivyo kazi nyingine za Fasihi, hutumiwa kwa lengo la kuasa, kuadibisha, kufunza, kujenga utafiti, ukombozi, kuburudisha, kustarehesha, kuhifadhi amali na kurithisha amali za jamii. Thamani ya nahau inapatikana kutokana na ujumbe pamoja na kuiakisi jamii katika mwelekeo wake wa

kiutamaduni na mambo mengine yanayohusiana na shughuli za kimaisha za kila siku. Nahau kwa kawaida hushughulikia masuala ya kijamii kwa mitazamo mbalimbali tangu mwanadamu anapozaliwa, kulelewa na hata kukua, shughuli zake na hata mwisho wa maisha yake. Kadharika, matumizi ya nahau hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine kulingana na mazingira yanayozingatia mahitaji ya kimafunzo. Nahau hutumika kwa kuzingatia mahitaji ya kimazingira, aina ya mafunzo na njia au mbinu inayotumika katika uwasilishaji.

2.3 Mapitio Kuhusu Taswira kwa Ujumla

Taswira au jazanda huambatana na matumizi ya tamathali za semi, hasa za sitiari na tashibiba,

Wamitila (2003) anasema kuwa:

Taswira ni aina mojawapo ya tamathali za usemi ambayo ina maana iliyofichika. Matumizi ya tamathali za usemi yamezoeleka sana sio tu katika riwaya au kazi za kifasihi, bali pia katika lugha ya kawaida. Taswira zimejengeka katika maumbo mbalimbali ambayo hutoa maana tofauti tofauti kulingana na mwandishi anavyozichora ili kutoa maana iliyokusudiwa. Kuna taswira zinazotokana na maelezo hizi hazina maana ya ziada nyingine na taswira za kiishara hizi huwa na maana ya ziada.

Hivyo, andiko hili limetuonesha kuwa kazi yoyote ya Fasihi ni lazima itumie taswira, kwani Fasihi bila ya matumizi ya taswira haimfanyi msomaji au msikilizaji kuweza kuonja, anuse, aone, achukie au afurahi. Na uhakiki usiozingatia taswira huifanya kazi ya Fasihi kuonekana kuwa ni chapwa. Vilevile hili lilimwezesha mtafiti kuzichambua taswira mbalimbali zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa.

Mulokozi (1989: 193-194) anasema kuwa, “Picha ni uwakilishaji wa jambo kwa kutumia kauli au maneno yanayosawiri picha au hali ya jambo hilo na kuibua hisia au vionjo kuhusu jambo hilo katika akili za msomaji au msikilizaji”. Hivyo basi,

athari tuzipatazo katika fikra zetu hutokana na uchoraji mzuri wa picha unaotumia lugha yenye ustadi wa hali ya juu na kuleta taswira fulani kwa hadhira. Pia andiko hili lilimsaidia mtafiti kuzichambua taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa pamoja na athari zake kwa jamii.

Miongoni mwa waandishi waliochambua suala la matumizi ya taswira katika kazi za Fasihi ni pamoja na Kahigi na Mulokozi (1982). Wakitumia msamiati wa picha wanasema:

Kwa kutumia picha mwandishi anaweza kumfanya msomaji wake asisimke, aogope, afurahike, ingawa matumizi ya lugha huweza kuzindua hisi na maono fulani katika akili ya msomaji au msikilizaji juu ya kile kinachozungumzwa

2.3.1 Matumizi ya Taswira

Kusaidia kuvuta taswira ya kitu kinachozungumzwa na kikakamata katika akili ya mtu kwa namna ya ajabu. Hakuna kitu kilicho na nguvu ya maoni katika usemaji, kama lugha ya taswira (picha). Husaidia sana kuvuta hisia na kuleta mguso wa hali ya juu kwa upande wa wenye kufikiwa na ujumbe. Lugha ya picha ni nguzo muhimu ambayo mtafiti anaamini kuwa ndiyo inayoshikilia matendo ambayo yamejenga wazo katika dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa.

2.3.2 Aina za Taswira

Kwa mujibu wa Senkoro (1982:13) zipo aina mbalimbali za taswira, nazo ni kama ifuatavyo:-

i/ Taswira ya hisi

Hizi zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kunasisha ujumbe wa mwandishi kwa wasikilizaji au wasomaji. Hizi hushughulikia hisia za ndani, na huweza kufanya

msomaji au msikilizaji awe na wasiwasi, aone woga, apandwe na hasira au asikie kinyaa.

ii/ Taswira za mawazoni ama kufikirika

Hizi zinatokana na mawazo, mawazo hayo ni yale yanayohusu mambo yasiyoweza kuthibitika. Mambo kama kifo, pendo, uchungu, fahamu, sahu na raha.

iii/ Taswira zionekanazo

Picha hizi hujengwa kwa kutumia vielelezo tunavyovijua na vinavyofahamika katika maisha ya kila siku.

Wamitila (2008) Naye anasema:

Taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Je, picha hizo hutokana na nini? Picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazotumia. Kuna taswira zinazotokana na maelezo ambazo hazina maana nyingine ya ziada. Hizi hujulikana kama taswira za kimaalezo. Zipo taswira ambazo huwa na maana nyingine ya ziada (yaani sio ile picha tu kuna ujumbe wa ziada). Hizi nazo huitwa taswira za kiishara, kama tunavyojua kuwa binadamu ana hisia mbalimbali. Picha zinazopatikana katika kazi za kifasihi huweza kulenga kuchochea kutazama, kunusa, kuonja, na kusikia.

Kutokana na msingi huu, tunapata aina mbalimbali za taswira au jazanda. Wamitila ameanisha aina za taswira kama ifuatavyo:-

i/ Taswira za uoni: Picha inayojengwa inalenga mtazamo wa macho.

ii/ Taswira za mnuso / harufu: Picha zinazojengwa zinalenga viungo vya harufu.

iii/ Taswira za mguso: Huleta picha ya hali ya kugusa kitu au vitu fulani kugusana.

iv/ Taswira za mwonjo: Hizi hujengwa kwenye hisia za kuonja. Kwa mfano kama maelezo yanayohusiana na chakula.

vi/ Taswira za usikivu: Msanii analenga hisia za kusikia kwa kujenga picha zinazohusiana na sauti.

vii/ Taswira ya mwendo: Hizi ni zile zinazotuletea picha ya mwendo.

viii/ Taswira ambazo kinaakisi hali ya hewa kama joto na baridi: Picha zinazohusiana na joto humjia msomaji. Yaani picha zinajengwa kwa matumizi ya maneno yanayohusiana na joto.

Msingi wa kutumia taswira au jazanda (na umuhimu wake pia). Kwa njia hii mwandishi anaupitisha ujumbe wake kwa nguvu zaidi na kazi yake inakuwa na mvuto mkubwa wa kisanii.

Hata hivyo, wamebaini kuwa picha huiwezesha hadhira kupata ujumbe uliokusudiwa wa kazi ya Fasihi, kwa kuzifafanua na kuzichambua picha zilizotumika. Pamoja na kuwa maelezo hayo yanatupatia mwangaza juu ya matumizi ya taswira katika kazi ya Fasihi, waandishi wanaonekana kuzungumzia zaidi Fasihi andishi katika utanzu wa ushairi tu, hivyo, kutuachia maswali muhimu kuhusiana na matumizi ya taswira katika Fasihi simulizi hususani kipengele cha matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa

2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Ingawa Wataalam mbalimbali wameshughulikia na kufanya utafiti katika kipengele cha semi na vipera vyake ikiwemo nahau, tumegundua kuna mapengo yafuatayo; kwanza, wengi wa wataalam hao wamezishughulikia nahau kwa kuzikusanya na kuangalia maudhui yake, hata hivyo, hawakukishughulikia kipengele cha taswira. Aidha, uchunguzi wao umejigeza katika nahau za Kiswahili na lugha nyingine lakini sio lugha ya Kisambaa.

2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Katika sehemu hii imekusudia kubainisha taswira ya jumla kuhusu machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada hii. Machapisho hayo yaliweza kugawiwa katika makundi makuu mawili, la kwanza lilihusiana na maandiko yaliyogusia semi. Pili ni maandiko kuhusu taswira katika Fasihi kwa jumla, sura inayofuata itajadili kuhusu usanifu wa mbinu na vifaa vya utafiti.

SURA YA TATU

USANIFU WA MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii imefafanua mpango wa jumla wa utafiti huu, eneo la utafiti, mbinu za kukusanyia data, zana na vifaa vya utafiti, jamii ya watafitiwa, mchakato wa ukusanyaji na uchambuzi wa data na uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti.

3.1 Mpango wa Utafiti

Kothari (2008) amefafanua mkabala wa utafiti kuwa:

Ni mpangilio mzima wa ukusanyaji na uchambuzi wa data katika hali inayoelekeza malengo ya utafiti na namna yatakavyofikiriwa. Kwa kawaida muelekeo wa utafiti huweza kuwa uchambuzi wa kifafanuzi au wa kimahesabu kutegemea na asili ya mada husika ambayo ndio inayomfanya mtafiti aamue kutumia muelekeo upi wa kiuchambuzi wa data.

Hata hivyo, mtafiti hulazimika kutumia mikabala yote miwili kwa pamoja pale inapobidi. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mkabala wa uchambuzi wa kifafanuzi (qualitative) ambao kimsingi si wa kimahesabu katika kukusanya data. Mkabala huu umeteuliwa kutokana na ukweli kuwa mada husika si ya kimahesabu.

Mulokozi (2003:17) anaeleza kuwa, “utafiti wa Fasihi simulizi una sehemu mbili, sehemu ya uwandani na sehemu ya maktabani”. Hivyo, utafiti huu umetumia utaratibu huo wa uwandani na maktabani katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Kwa sehemu ya uwandani watafitiwa walipewa dodoso zilizowaongoza kujibu maswali ya utafiti huo. Mbinu nyingine iliyotumika katika mchakato wa kukusanya data ni majadiliano na mahojiano baina ya mtafiti na mtafitiwa na mapitio mbalimbali ya vitabu kutoka maktabani. Data zilizokusanywa kutoka katika

maandiko mbalimbali yanayoelezea fani katika nahau pamoja na mahojiano kutoka katika jamii ya Kisambaa zilihakikiwa kwa kuzingatia nadharia ya Umuundoleo.

3.2 Jamii ya Watafitiwa

Jamii ya watafitiwa hujumuisha wale wote ambao mtafiti anadhani kuwa wanaweza kutoa taarifa zinazofaa katika malengo ya utafiti wake. Hivyo, utafiti huu ulifanyika Mkoani Tanga, katika Wilaya ya Lushoto hasa kuhusiana na data za uwandani. Data za maktabani zilipatikana katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma iliyopo Mkoani Dodoma, Maktaba ya mkoa ya Dodoma na Maktaba ya Taifa iliyopo Mkoani Dar es Salaam na kazi nyingine zinazohusiana na mada ya utafiti huu zilipatikana kwa njia ya mtandao.

3.2.1 Walengwa wa Utafiti

Shulman (1988:14) anaeleza kuwa “walengwa wa utafiti ni kundi la watu, vitu, au asasi zinazoelezea kuhusu vitu vinavyofanyiwa utafiti”.

Utafiti huu ulilenga makundi ya aina mbili;

(i)Wazawa wa kabila la Kisambaa waishio katika tarafa ya Soni

(ii)Wasomi wa Fasihi.

3.2.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji wake

Kothari, (2008:4-24), “Sampuli ni sehemu ndogo ya jamii ambayo huteuliwa na mtafiti ili aitumie katika kukusanyia data”. Ukubwa wa sampuli huteuliwa kulingana na aina ya utafiti na nyenzo alizonazo mtafiti kama vile fedha na muda wa kuendeshea utafiti. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa.

Katika utafiti huu nahau thelathini na tano (35) zilitumika katika kufanya uchambuzi. Idadi hii kubwa ya nahau imetokana na ukweli kuwa tafiti za kitaamuli huhitaji sampuli kubwa ikilinganishwa na tafiti za kitakwimu.

Kombo na Tromp, (2006:82) anaeleza kuwa; “Sampuli lengwa ni sehemu ndogo ya jamii ya watafitiwa ambayo huchaguliwa na mtafiti kwasababu huwa na sifa zinazokidhi mahitaji ya utafiti”. Mbinu hii ya sampuli lengwa inafaa zaidi katika tafiti za kitaamuli kama hizi ikilinganisha na zile za kitakwimu.

Wawakilishi walichaguliwa kulingana na jinsi walivyoweza kukidhi mahitaji na malengo ya utafiti huu; na walichaguliwa kutoka katika makundi yote yanayounda wango jamii ya watafitiwa. Hivyo, vigezo vikubwa vilivyotumika katika kuwapata vilikuwa ni viwili – miongozo ya kinadharia kutoka kwa wataalamu wa nadharia ya utafiti (Kothari, 2009). Pamoja na asili ya utafiti wenyewe (kwamba ni wa kitaamuli na unahusisha Fasihi simulizi na jamii). Ili kukidhi mahitaji ya utafiti huu wawakilishi waliohojiwa walikuwa 30 wa ngazi mbalimbali. Kama ifuatavyo:

(a)Wazee waishio eneo la utafiti (Soni) 15

(b)Wanachuo 15 wa shahada ya kwanza wanaojifunza taaluma ya Fasihi simulizi katika Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa (SEKOMU). Hivyo, watafitiwa hawa walitokana na asili ya mada yenyewe, kwani ilihitaji data kutoka kwa wajuzi wa Fasihi simulizi, pia vitabu vya Fasihi vinavyoelezea nahau kwa ujumla vilitumika.

3.3 Ukusanyaji wa Data

Kipengele hiki kilihusu njia na zana mbalimbali zilizotumika katika mchakato wa ukusanyaji data.

3.3.1 Zana za Kukusanyia Data

Kwa mujibu wa Mulokozi (2003:13) anaonesha kuwa; “zana za kukusanyia data hutegemea mada, shabaha za utafiti, uwezo wa mtafiti kitaaluma na kifedha na hata kimazingira na kitamaduni”. Vilevile, utafiti huu ulitumia zana ambazo ni pamoja na karatasi, daftari, kalamu na kamera ya picha mgando. Pia kinasa sauti ni zana nyingine iliyotumika kuchukua data za washirika ambao hawawezi kunukuu. Vitabu, majarida na tasnifu mbalimbali ni zana za maktabani zilizosaidia kuvuna maarifa yaliyohusiana na mada ya utafiti. Data za mtandaoni kupitia tovuti mbalimbali pia zilisaidia kupanua maarifa katika mchakato wa utafiti wa mada hii.

3.3.2 Njia ya Kukusanyia Data

Utafiti huu ulitumia zaidi njia ya mahojiano kama asemavyo Kothari (2008: 272) “mahojiano ni mpangilio mzima wa maswali maalum yenye lengo la kukusanya taarifa”. Njia nyingine iliyotumika ni dodoso na majadiliano katika vikundi lengwa ili kupata data zilizokusudiwa. Hivyo ufafanuzi wa njia hizo ni kama ifuatavyo:-

3.3.2.1 Dodoso

Dodoso ni kifaa cha ukusanyaji wa data ambayo mtafitiwa ndiye hujaza majibu kulingana na utafiti unavyo hitaji. Dodoso inatokana na neno dodosa ambalo lina “maana ya kudadisi mtu kwa kumuuliza maswali” TUKI, (2004: 235-240). Mtafiti alitumia dodoso kwa wazee wasomi waishio katika tarafa ya Soni kwenye vitongoji husika, kwa kujaza dondoo ya maswali waliyopewa kulingana na mada husika. Hivyo mbinu hii ya dodoso iliweza kumsaidia mtafiti kujua nahau mbalimbali za Kisambaa kutoka kwa wazee. Pia, mbinu hii iliweza kumnufaisha mtafiti kwani aliweza kupata nahau kadhaa zilizomwezesha kuandaa utafiti huu.

3.3.2.2 Mahojiano

Hii ni karatasi yenye maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa lengo la kumhoji mtafitiwa. Maswali haya yanafungamana na malengo ya utafiti husika. Mtafiti alitumia maswali hayo kama mwongozo wake katika kupata data husika kutoka kwa mtafitiwa. Hivyo, mahojiano yalimwezesha mtafiti kupata data za msingi na fuatizi. Mahojiano yaliyotumika katika utafiti huu yameambatishwa mwishoni pamoja na viambatishi vingine.

3.3.2.3 Mjadala wa Vikundi

Mjadala wa vikundi ni njia mojawapo ambayo mtafiti alitumia kukusanyia data katika utafiti huu. Katika njia hii mtafiti hulazimia kuwagawa watu katika makundi ya watu kadhaa na kupata kiongozi kwa kila kundi wa kuweza kusimamia mjadala huo, vilevile mtafiti hulazimika kuwepo akizulu kila kundi ili kutoa msaada pale inapobidi. Lengo hasa la mtafiti kuitumia njia hii ni kuweza kuwapa uhuru zaidi watafitiwa wa kuweza kueleza nini wanafahamu kuhusu mada hii wakiongozwa na dondoo ya maswali kutoka kwa mtafiti. Hivyo, mbinu hii ilisaidia sana katika ukusanyaji na upatikanaji wa data za utafiti.

3.3.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti wake

Utafiti huu ulizingatia maadili ya utafiti, mtafiti aliomba kupatiwa barua ya ruhusa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ili kuweza kupata ridhaa ya kukusanya data katika taasisi mbalimbali na kwa wahojiwa. Pia mtafiti alikutana na watafitiwa wake kisha akajitambulisha na kueleza lengo la utafiti wake, vilevile aliomba ridhaa ya watu aliotaka kuhojiana nao na kuwashirikisha katika utafiti huu. Na mtafiti aliwahakikishia watafitiwa kuwa taarifa walizozitoa zitatumika kwa madhumuni ya utafiti tu na si vinginevyo, na kwamba taarifa zao binafsi zitabaki kuwa siri, hivyo,

maadili ya uendeshaji utafiti yalizingatiwa. Data za maktabani zilikusanywa kupitia udurusu wa majarida, vitabu, tasnifu na makala mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti. Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya dodoso, mjadala vikundi na mahojiano ambapo mwongozo wa njia zote tatu ulitumika. Mwongozo wa mjadala wa vikundi ulitumiwa kwa wanafunzi wa Shahada ya kwanza ya Fasihi ya Kiswahili, mtafiti aliwagawa watafitiwa katika makundi matatu na kila kundi lilikuwa na watu 5 tu, pia kila kundi lilikuwa na kiongozi wao ili kurahisisha shughuli ya ukusanyaji data na pia njia hii iliwapa uhuru watafitiwa kuweza kujieleza zaidi. Mtafiti alikuwa akizulu kila kikundi ili kuweza kuona kazi inaendelea na kuweza kutoa msaada kwa watafitiwa pale ilipobidi. Madodoso yalitumika kwa wazee (wasomi) ambao ni wazawa wa kabila la Wasambaa ili kuweza kupata data zilizokusudiwa. Mahojiano yalitumiwa kwa wazee (ambao sio wasomi), mtafiti alikutana ana kwa ana na kuweza kuhojiana na wazee hao akiongozwa na jedwali la maswali lililoandaliwa kwa shughuli ya utafiti ili kuweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

3.3.4 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Mtafiti alichanganya mbinu ili kuona namna ambavyo data zilizokusanywa jinsi zilivyoweza kufanana hata kama alitumia mbinu tofauti. Matumizi ya mbinu mchanganyiko yalimsaidia mtafiti kupata data zilizoweza kurandana kwa kiasi fulani, pia mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa thabiti na mtafiti kupitia njia hii alihakikisha kuwa matokeo ya data hayatoki nje ya malengo yaliyokusudiwa katika utafiti. Pia zana na vifaa vilivyotumika vilikusudia kupima kile kilichokusudiwa kupimwa katika utafiti huu kwa lengo la kupata uhalali na umakinifu wa data.

3.4 Uchanganuzi wa Data

Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa ni wa kitaamuli, ukusanyaji, uchanganuzi na Utoaji wa matokeo ulifanyika kwa mfumo wa maelezo. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mhimili wa nadharia ya Umuundoleo. Uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Kwa hiyo, kila lengo lilitarajiwa kuunda maudhui yaliyoendana na mada ya utafiti. Data zilikusanywa kupitia dodoso, majadiliano na mahojiano baina ya mtafiti na mtafitiwa zilijumuishwa na zile zilizopatikana kupitia udurusu wa maktabani na baadaye zilipimwa na kutathiminiwa. Huku kulisaidia kuongeza ubora na uthibiti wa matokeo. Baada ya uchanganuzi huo, matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya ufafanuzi. Njia nyingine iliyotumika kutoa matokeo ya utafiti huu ni ya vielelezo.

3.5 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imeelezea kwa kina mbinu mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika zoezi la ukusanyaji wa data. Mambo yaliyowasilishwa ni pamoja na eneo la utafiti ambalo data zilipatikana, walengwa wa utafiti huu, mchakato mzima wa ukusanyaji data, njia za kukusanyia data, mbinu za kukusanyia data, ambazo ni mahojiano mjadala wa vikundi pamoja na dodoso, maktaba. Pia, vifaa vya vilivyotumika ambavyo ni kamera, simu ngamizi vimeanishwa na kufafanuliwa. Vilevile, mchakato wa uainishaji na uchambuzi wa data baada ya kukusanywa umeelezwa katika sura hii. Mwisho kabisa mipaka ya utafiti pamoja na maadili ya utafiti yamefafanuliwa vema.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili matokeo ya utafiti, mjadala umegawanyika katika sehemu kuu tatu zinazoakisi malengo na maswali yaliyotumika kuongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza, inajadili namna taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa, Sehemu ya pili, inajadili na kutathimini athari zinazojitokeza katika ufafanuzi na uelewekaji wa taswira katika nahau za Kisambaa kwa hadhira. Sehemu ya tatu, imechambua uhusiano uliopo baina ya matumizi ya taswira katika nahau na maisha halisi ya jamii.

4.2 Taswira Zinavyojitokeza katika Nahau za Kisambaa

Fanani hutumia maneno ambayo hujenga umbo la kitu akilini mwa hadhira. Taswira ni picha ziundwazo akilini mwa msomaji au msikilizaji kutokana na maelezo yanayotolewa na msemaji. Ni hali ya kueleza jambo au kitu hadi wasomaji au wasikilizaji wakakiona kwa urahisi kabisa katika akili zao.

Nahau za Kisambaa zina matumizi makubwa ya taswira, kusambaa kwa nahau katika vipengele mbalimbali vya maisha ya binadamu ni kusambaa kwa taswira pia. Hivyo, kitu chochote chenye uhusiano na maisha ya binadamu pia kinaweza kuwepo kwenye nahau, hatimaye kuwemo kwenye taswira kwa ajili ya kutoa ujumbe fulani katika jamii, vilevile mazingira yanayomzunguka binadamu yanahusika sana katika kujenga taswira akilini mwake.

Taswira zinazochomoza katika nahau za Kisambaa tunazipata pale fanani anapozungumza na jamii ili kuweza kuifikia kwa urahisi. Hivyo, katika nahau hizo

tunapata aina mbalimbali za taswira kama vile taswira za kuonekana, taswira za kufikirika, taswira za kugusa, taswira za hisi na hata za kunusa pia.

4.2.1 Taswira za Kuonekana

Taswira hizi hujengwa kwa kutumia vielelezo tunavyovijua na vinavyofahamika katika maisha ya kila siku katika mazingira watu wanamoishi. Mfano katika nahau hizi hapa chini;

(a) *Mashafi yana nda, fisha mbui ya sii*

Kiswahili: **Vichaka** vina **mimba**, fisha jambo la siri

Maana yake: Tusiseme siri zetu kila mahali kwani watu wengine watasikia na kuzifikisha mahali ambapo hazikupaswa kufika.

Taswira: Vichaka na mimba

Katika nahau (a) *mashafi yana nda*. Taswira inayopatikana hapa ni ya kuonekana, ambayo ina **vichaka** na **mimba**, vichaka vinaashiria mahali palipojificha na mimba inaashiria jambo la siri. Inalinganishwa na vitu vinavyoonekana ambavyo vipo katika ulimwengu halisi, na vitu hivyo hupatikana katika mazingira halisi wanayoishi Wasambaa. Katika nahau hii tunapata taswira kuwa vichaka vina mimba kwa maana kuwa, tusiseme siri zetu kila pahali kwani wapo watu watasikia siri hizo na kuanza kuzisema pahali ambapo hazikustahili kusemwa na kusikika katika sehemu hizo zisizohusika hatimaye zikaleta uhasama. Hivyo, vichaka na mimba vinapotajwa katika muktadha wa kiubunifu mtu anafikiria taswira anayoipata ni ya namna ya kuhifadhi siri na sio kuisema hadharani, kwani wengine wanaweza kusikia na ikawa sio siri tena. Vivyo hivyo, vitu hivi vinapotajwa katika muktadha huu wa kifasahi na kupangwa kwa ubunifu basi vinaleta fikra mpya na taswira mpya akilini

mwa msomaji au msikilizaji. Na hivyo, mwanadamu anapata nafasi ya kutafakari juu ya mazingira yake na kuyaeleza kwa upya.

*(b) Kukong'wa **nzisho** jako, kushaghua kitnu kibaya*

Kiswahili: kuponzwa na **jicho** lako, fanya uamuzi usio sahihi

Maana yake: Mtu akishindwa kuchagua kitu kizuri kati ya vitu vingi huambiwa nahau hiyo kwa kumaanisha kuwa alishindwa mwenyewe kufanya maamuzi sahihi.

Taswira: jicho

Nahau (b) hapa tunapata taswira ya kuonekana, taswira ya **jicho**, kama tunavyofahamu katika mazingira ya kawaida, tusikiapo neno jicho wote tunajua kuwa ni kiungo cha mwili kati ya milango mitano ya fahamu na kazi yake ni kuona. Katika nahau hii tunapata kufahamu kuwa neno hili limetumika tofauti na tunavyolifahamu, limetumika katika kutoa uamuzi. Mtu anaposhindwa kuchagua kitu kizuri kati ya vitu vingi huambiwa nahau hiyo kwa kumaanisha kuwa alishindwa mwenyewe kufanya maamuzi sahihi. Hivyo, hapa taswira chomozi ni ya jicho kama kiungo kitumikacho kuchagua kitu sahihi ambacho kinamfaa mtu kukitumia. Mtu akiisikia nahau hii katika mazungumzo ya kawaida anaweza asielewe maana yake, lakini neno hilo likisukwa kwa ufundi wa kifasihi hadhira hupata dhana mpya akilini mwake.

*(c) Kuja **kagoghwe**, kuhenya mbui*

Kiswahili: kula **gogwe**, kudanganya

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kuongeza au kukuza jambo kwa kuongeza maneno ya uongo ndani ya habari anayopaswa kuifikisha mahali fulani.

Taswira: gogwe

Katika nahau (c) taswira tunayoipata hapa ni taswira ya kuonekana, taswira ya **gogwe** ambayo huashiria maneno ya uongo au yaliyotiwa chuku, kwani kazi ya tunda hili katika jamii ya Wasambaa ni kuchachusha mboga ili kuifanya inoge zaidi na iweze kuleta radha nzuri wakati wa kula. Neno hili linapotajwa katika ufundi wa kifasihi msikilizaji ama mzungumzaji anapata dhana ya kitu kingine, tofauti na linapozungumzwa katika mazingira ya kawaida. Hapa ndipo nadharia yetu ya Umuundoleo inapoweza kutumika katika matumiza ya lugha ya kuweza kupata maana kulingana na muktadha.

(d) *Kughosha ndima ya **gunda**, ndima ishinayo maiho*

Kiswahili: Kufanya kazi ya **msaragambo**, kazi isiyo na tija.

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kufanya kazi isiyo na tija, kwani siku zote tunatarajia kufanya kazi ambazo zinatupatia kipato ili kuendesha maisha yetu.

Taswira: baragumu

Katika nahau (d) *kughosha ndima ya **gunda***, taswira tunayoipata hapo ni ya kuonekana taswira ya kifaa kinachoitwa **baragumu**, kwani kifaa hiki kitajwapo katika jamii hii watu hupata dhana ya kwenda kufanya kazi ya msaragabwe. Neno gunda limetumika kumaanisha kufanya kazi isiyo na tija inayofananishwa na kazi ya msaragambo. Neno hili linapozungumzwa katika ufundi wa kifasihi huweza

kumfikirisha msikilizaji ama msomaji na hapa huweza kupata dhana mpya ya mtu kufanya kazi isiyo na faida. Hivyo, nahau hii inapotajwa hadhira anapoisikia hupata dhana mpya katika fikra kulingana na muktadha wa mazungumzo. Kwani neno hili likitumika katika mazingira ya kawaida mtu hawezi akaelewa kwa urahisi nini fanani amekusudia, lakini likisukwa katika ufundi wa kifasihi mtu huweza kufikiri kwa kina zaidi ili kupata sura ya kile fanani alichokusudia.

(e) *Kuja **kaoka**, kuja sungu mwe ndima*

Kiswahili: kula **kitu cha kuchoma**, kupata shida

Maana yake: Ili mtu afanikiwe katika jambo fulani hana budi kupitia katika shida na taabu nyingi, ili kufikia lengo anatakiwa kuwa mvumilivu.

Taswira: shida, ugumu wa kupitishwa katika moto.

Katika nahau (e) *kuja **kaoka***, taswira chomozi hapa ni ya hisi na ya kuonekana, **kitu kilichochochomwa** ndio taswira tunayoipata katika neno hili likimaanisha shida na adha apatazo mtu ili kufanikiwa katika jambo, hivyo kitu kilichochochomwa huonekana kuwa imara na bora zaidi kuliko kilichochemshwa. Vile vile, neno hili linapozungumzwa katika mazingira ya kawaida mtu anaweza kuelewa kuwa mtu fulani anakula kitu kilichochochomwa. Lakini neno hili likizungumzwa katika ufundi wa kifasihi basi hadhira huweza kufikiri kwa kina zaidi na kupata dhana mpya ya taswira iliyochochoza ndani yake ya mtu kupata shida na adha nyingi katika kufanikisha jambo fulani.

(f) *Mntu **mbughe**, mntu mwena choyo*

Kiswahili: Mtu **mbuge**, mtu mchoyo

Maana yake: Ni tabia ya uchoyo aliyonayo mtu kupenda kupokea vitu kutoka kwa wengine wakati yeye ni mgumu katika kuwapatia wengine.

Taswira: Mbuge

Nahau (f) *mntu mbughe* taswira tuiapatayo hapa ni taswira ya kuonekana. Taswira ya mnyama aitwaye **Mbuge** ambaye amebeba dhana ya tabia ya uchoyo na ubinafsi, mtu anayependa kupokea vitu toka kwa wengine ila yeye ni mgumu wa kutoa. Katika jamii hii mtu akisikia neno hili hupata taswira hiyo. Hivyo, neno hili limefumbwa kisanaa, kwani linapozungumzwa katika mazingira ya kawaida mtu huweza kufikiria kuwa mzungumzaji alikuwa na maana ya mnyama. Hata hivyo, likisukwa katika ufundi wa kifasihi basi hadhira huweza kufikiri kwa kina ili kuweza kulifumbua fumbo alilofumbiwa na kuweza kupata dhana mpya ya mtu mchoyo. Katika jamii hii mtu mchoyo huitwa mbughe ili kufumba maneno kwa kufananishwa na mnyama huyo mwenye tabia ya uchoyo.

4.2.2 Taswira za Kufikirika

Hizi zinatokana na mawazo, mawazo hayo ni yale yanayohusu mambo yasiyoweza kuthibitika. Mambo kama kifo, pendo, uchungu, fahamu, sahau na raha, mfano wa taswira za kufikirika tunazipata katika nahau zifuatazo:-

(a) *Kuita uzozo, kutozeezwa viugho n' nyao*

Kiswahili: Kutekwa ufahamu/akili, Kupumbazwa akili kwa soga za wengine

Maana yake: Ni kile kitendo cha mtu kutekwa ufahamu na kupumbazwa kwa soga za wengine.

Taswira: Akili

Katika nahau (a) taswira inayochomoza hapa ni ya kufikirika ni ya mtu kutekwa ufahau kimazingala, ikiwa na maana ya mtu kupumbazwa ufahamu kwa soga za wengine zisizo za msingi. Neno hili inapozungumzwa katika mazingira ya kawaida mtu hawezi kuelewa kusudio la mzungumngumzaji, lakini ikizungumzwa katika muktadha huu wa kiubunifu katika Fasihi basi fanani huweza kufikiri ni nini kusudio la fanani katika kutumia ufundi huo wa maneno.

(b) Kutana na ubweni, n'kughua mvyee

Kiswahili: Kuachana na ukapera, kupata **jiko**, kuoia mke

Maana yake Kuoia au kupata mke

Taswira: Jiko

Katika nahau (b) taswira tuiapatayo hapa ni ya kufikirika, taswira ya **jiko** inayoashiria mke, ni dhahiri kuwa katika maisha ya kawaida mwanaume akipata mke amepata mtu wa kumsaidia katika shughuli mbalimbali za kimaisha hususani za jikoni kama vile kumpikia, kufagia na kuosha vyomba. Pia inawezekana kijana alikuwa na jiko kama kifaa, lakini kwa wakati huo hakuwa akilitumia katika kupikia kutokana na kutojua kupika ama pilikapilika za maisha hata kukosa muda huo hatimaye kwenda kwa mama ntiliye au migahawani ili kupata chakula. Hivyo, neno hili likizungumzwa katika maongezi ya kawaida msikilizaji anaweza asielewe lengo la mazungumzo hayo, akafikiria amepata jiko kama kifaa cha kupikia chakula kumbe sivyo. Lakini neno hili likisukwa kisanaa katika Fasihi hubadilika na kuwa nahau,

ambayo huweza kumfikirisha hadhira hata kuweza kung'amua fumbo alilofumbiwa na fanani wake katika mawasiliano yao ya kiusemaji. Hadhira anaweza kupata maana halisi au inayowezezana kulingana na muktadha wa mazungumzo yao na hupata dhana mpya akilini mwake ya mtu kuoja mke.

Hivyo, katika nahau hizi tumeona kuwa kipengele cha taswira katika matumizi ya lugha ni muhimu sana, kwani huleta uhai katika kazi ya kifasihi. Vilevile huifanya kazi hiyo isionekane kuwa ni chapwa na kuweza kuleta mvuto kwa hadhira.

4.3 Athari ya Taswira katika Nahau za Kisambaa katika Ufafanuzi na Uelewekaji Wake kwa Hadhira

Katika Fasihi simulizi nahau ni kipengele muhimu ambacho hubeba mafumbo yenye kuhitaji kufumbuliwa na hadhira. Binadamu katika ulimwengu huu amezungukwa na mambo mengi anayoyafahamu, yale yanayoonekana na yasiyoonekana pia ambayo humsaidia kuyafumbua mafumbo mbalimbali yatumikayo katika kuunda nahau. Hivyo, nahau inapofumbwa huchochea taswira fulani akilini mwa hadhira ambayo anaihusisha na kuilinganisha na vitu kadhaa avionavyo katika ulimwengu halisi, miongoni mwa vitu hivyo huweza kupata vinavyorandana zaidi na taswira aliyoipata kupitia maneno yaliyotumika kuunda nahau hiyo.

Zipo athari mbalimbali ambazo zaweza kujitokeza katika matumizi ya nahau, athari hizo zaweza kuwa chanya au hasi kulingana na utokeaji wake kama ilivyo katika maelezo haya yafuatayo:-

4.3.1 Athari Chanya

Taswira zinazochomoza katika nahau za Kisambaa humfikirisha hadhira na kuanza kuutazama ulimwengu kwa upya, tofauti na alivyokuwa akiutazama hapo mwanzo.

Mtazamo huo mpya aupatao hadhira hutokana na matumizi ya kiishara yaani kiashiria na kiashiriwa, hivyo, hadhira huweza kupata maana ya neno kwa kuweza kung'amua kile kilichotajwa akilinganisha na kilichorejelewa ndani ya fumbo hilo, kulingana na matumizi ya vitu ambavyo hupatikana katika mazingira halisi anamoishi. Hivyo, hadhira anaweza kufumbua fumbo alilofumbwa kwa kuhusianisha kiashiriwa pamoja na taswira inayopatikana na vitu halisi vilivyomo katika ulimwengu halisi. Taswira zinazopatikana wakati vitu hivyo vitajwapo katika ufundi wa kifasihi huonesha upekee wake tofauti na pale ambapo vitu hivyo vinapotajwa katika maneno ya kawaida. Hivyo, katika utafiti huu imeonesha kuwa watafitiwa wengi walijibu kuwa moja ya faida zipatikanazo katika utumiaji wa taswira katika nahau za Kisambaa ni kama ifuatavyo:-

4.3.1.1 Taswira Humwezesha Hadhira Kupata Undani wa Nahau

Kusikia neno ni hatua ya kwanza, bali kulifahamu neno ndiyo jambo muhimu. Katika lugha yeyote ile watu hutumia maneno kwa ufundi wa hali ya juu ili kufikisha ujumbe kwa jamii au hadhira iliyokusudiwa. Kutokana na nahau hizo kutumia lugha ya picha au mafumbo, kwa kawaida ni wanajamii wachache wenye upeo wa kuweza kupata undani wa nahau hizo pindi zitumikapo, kwani taswira mara nyingi huficha jambo la siri kutofahamika kwa wengine ambao hawahusiki. Katika utafiti uliofanywa na mtafiti imebainika kuwa mbali na wanachuo pamoja na wanajamii watumiao nahau za Kisambaa, ni watumiaji wacheche tu wa nahau wenye upeo wa kuweza kufikiria na kugundua maudhui ya taswira katika nahau hizo. Hivyo, tathimini inaonesha kuwa si watu wengi wanaoweza kugundua undani wa nahau hizo pindi zitumikapo. Ni wachache wanaoweza kufikiri na kufika mbali ili kupata dhana mpya katika fikira zao. Ni wazi kuwa hali hii inahitaji waledi wa lugha wanaoweza kuhangaisha akili zao katika kufikiri. Pia imeonesha kuwa, vijana wa

sasa wanataka kila kitu kwa uwazi bila kuhangaisha akili zao, wanaona kuwa utumiaji wa taswira katika kuufikisha ujumbe kwa hadhira umepitwa na wakati, kwani unawapotezea muda mwingi wa kukaa na kutafakari juu ya ujumbe ulio tolewa ili kupata kusudio la fanani. Hivyo, Idadi kubwa ya watu hasa vijana huzitumia tu kama kuipamba lugha bila ya kuelewa maudhui yabebwayo ndani yake. Mfano katika nahau zifuatazo:

(a) ***Kutoza funda**, n'kutozwa n'fanyanyi.*

Kiswahili: **Kushika shavu**, kuhuzunika

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kusikitika kwa kushika tama baada ya kusikia habari ambayo inaugusa na kuumiza moyo wake kwa majonzi na masikitiko.

Taswira: Hapa **kushika shavu** huashiria kitendo cha mtu kuhuzunika pindi asikiapo habari zinazoumiza moyo wake,

Katika mazingira ya kawaida hatutazamii kumwona mtu wakati wa furaha akiwa ameshika shavu ama wakati wa kupata habari njema ya kuufurahisha moyo wake tukamkuta ameshika shavu kwani hadhira itashangazwa na kitendo hicho.

Hivyo, neno hili humfikirisha hadhira ili kuweza kujua nini kusudio la fumbo alilofumbiwa na fanani wake ili kuweza kupata undani wake.

(b) *Gea **utambi**, kushongeeza mbui*

Kiswahili: Tia **utambi**, chochea

Maana yake: Ni kile kitendo cha mtu kulikuza na kulifanya jambo liwe kubwa lingali likionekana la kawaida, hivyo kulishadadia na kulifanya zito hatimaye kuleta mtafaruku ama ugonvi baina ya watu ndani ya jamii.

Taswira: Utambi

Katika nahau hii, tia **utambi** ni neno ambalo huashiria kitendo cha kuchochea jambo, kama tujuavyo kazi ya utambi ukichochea huwaka moto na hatimaye moto huo unaweza kuwaka kwa kasi zaidi hatimaye kuleta madhara kwa kuunguza mali na vitu vyote vinavyozunguka mazingira hayo. Hivyo, katika nahau hii ni hadhira wachache wanaoweza kung'amua na kupata undani wake kuwa jambo likikuzwa likawa kubwa linaweza kuleta athari katika jamii husika.

(c) *Kuvutika **mtwi**, kugimbikwa*

Kiswahili: Vimba **kichwa**, pata sifa

Maana yake: Sifa anayopewa mtu kupita kiasi humfanya ajione yeye ni bora zaidi kuliko wengine, hivyo kuanza kuwadharau wengine na kuwaona si kitu kwake.

Taswira: kichwa

Ndani ya nahau hii taswira chomozi ni ya mtu kuvimba **kichwa** huashiria sifa kupita kawaida apatazo mtu pindi afanyapo jambo fulani la ushindi na akapongezwa kupita kawaida kwa ushindi huo.

(d) *Haka **mikono**, kukiavya mwe mbui*

Kiswahili: **Nawa mikono**, kujitoa

Maana yake: Mtu anapofika hatua ya kughaili kuendelea kufanya majukumu aliyokuwa anafanya hapo awali, hivyo kutoendelea katika kulifanya jambo kwa maneno au vitendo vya kuvunjwa moyo.

Taswira: Nawa mikono

Katika nahau hii taswira chomozi ni ya **nawa mikono** ambapo huashiria kitendo cha mtu kujitoa katika kufanya jambo fulani ambalo alikuwa akilifanya hapo awali. Kama tujuavyo kitendo cha kunawa mikono hufanywa ili kutoa uchafu uliopo katika mikono kusudi iwe safi, hivyo kitendo hiki kifanyikapo mtu hufanya ili kujisafisha katika jambo fulani hatimaye kuepuka lawama katika jambo hilo.

*(e) Azatoza **uzumbe**, kuwaongoza wantu*

Kiswahili: Shika **usukani**, kuongoza

Maana yake: Ni hali ya mtu kuwa na jukumu la kuongoza watu katika jamii.

Taswira: Usukani

Katika nahau hii taswira chomozi ni ya kushika **usukani** ambapo huashiria dhana ya mtu kuwaongoza wengine, kama tujuavyo katika hali ya kawaida dereva ndiye mwenye jukumu la kuwaendesha abiria chomboni, ambacho katika nahau hii abiria ni wananchi wanaoongozwa na dereva mshika usukani ndiye kiongozi wao. Vilevile, inaonesha kuwa kiongozi naye ana maamuzi ya mwisho, kwani anajukumu la kuhakikisha kuwa kuna usalama, pia, kuhakikisha mambo yote yanaenda vizuri katika jamii husika.

Hivyo, ni dhahiri kuwa taswira husaidia hadhira kupata undani wa nahau kutokana na ufundi wa maneno namna yanavyosukwa kifasihi ndani yake. Hii huwafanya hadhira wachache kulitambua kusudio la fanani, hasa pale hadhira anapotaka kuficha jambo na kuufanya ujumbe wake kuwa siri, akitaka umfikie tu yule mlengwa aliyemkusudia, hapa huwafanya wasiohusika kushindwa kuelewa undani wake na kuishia tu kusikia ufundi huu wa maneno uliotumika. Hivyo, ufundi huu wa kisanaa huitajirisha na huipa upekee kazi ya fasihi tofauti na kazi nyingine zisizo za fasihi katika matumizi ya taswira katika lugha.

4.3.1.2 Taswira Hutusaidia Kuweka Kumbukumbu ya Kudumu Akilini mwa Msomaji ama Msikilizaji

Katika maisha ya mwanadamu kumbukumbu ni jambo la muhimu sana, kwani likikosekana husababisha nyaraka muhimu kupotea hususan katika taasisi fulani, vilevile husababisha mambo yasiende kama yalivyo tarajiwa hapo awali. Kumbukumbu hutusaidia kuyafahamu mambo ya nyuma ili tuweze kujifunza kupitia hayo kwa kuyarejelea hatimaye hata kuunda kitu kipya. Kumbukumbu hutusaidia kuijua hata historia ya lugha katika jamii zetu. Hata katika Taasisi mbalimbali zinakuwepo daftari ama vifaa mbalimbali kwa ajili ya kutunza mambo muhimu yatakayowasaidia hapo baadaye. Hivyo basi, hata katika kazi ya Fasihi matumizi ya taswira hutusaidia kutunza kumbukumbu katika akili zetu kupitia lugha ya picha inayotumika kujenga nahau hiyo. Hii inaonesha katika lugha matumizi ya taswira ni muhimu sana katika kazi ya Fasihi. Vilevile, matumizi ya taswira huipa kazi ya Fasihi uhai pale inapotumika na huifanya kazi hiyo kuonekana mpya kila siku kutokana na upekee wake katika ufundi wa maneno uliotumika, kwani katika kuufikisha ujumbe wake hurejelea vitu halisi vinavyofahamika na vimzungukavyo mwana jamii ambavyo si rasihi kusahaulika akilini mwake. Mfano katika nahau hizi:

(a) Ulimi wa uona, kuonga mbui ya mambeza ushieneyo

Kiswahili: Kusema maneno ya uongo, sema jambo ambalo hujalishuhudia kwa macho.

Maana yake: Kusema habari ya uongo ambayo hujaithibitisha kwa kuona.

Taswira: Ulimi

Katika nahau hii taswira chomozi ni ya **Ulimi** huashiria maneno ambapo katika nahau hii kuonesha utendaji wa kusema maneno ya uongo ambayo mtu huyanena pasipo kuthibitisha kwa kuyasikia yeye mwenyewe.

(b) Kuchungulia kabui/mbila, n'kuhuma kubua hehi na kufa

Kiswahili: Kuchungulia **kaburi**, kuugua mtu hata kukaribia kufa

Maana yake: Kuugua sana hata mtu kukosa matumaini ya kuishi tena.

Taswira: Chungulia kaburi

Katika nahau hii taswira iliyochomoza ni ya **kuchungulia kaburi** ambapo kaburi huashiria maumivu makali apatayo mtu wakati anapougua hadi kukata tamaa ya kuishi tena.

(c) Kumng'ata mtu gutwi, ni kumghambia mbui ya sii

Kiswahili: **kumng'ata mtu sikio**, kumnongoneza jambo

Maana: Kumwambia mtu jambo la siri kwa kumnong'oneza sikioni mwake.

Taswira: sikio

Katika nahau (c) kumng'ata mtu sikio, tunaona kuwa maneno yaliyotumika kuunda nahau hii yametumia taswira ambayo husadia pia kutunza kumbukumbu pale fanani anapoanza kutafakari ili kupata ujumbe. Kwani kitendo cha mtu kumwinamia

mwenzake sikioni na kuanza kucheza midomo yake wakati atamkapo maneno kwa sauti ya chini, kimefananishwa na kitendo cha mtu kucheza midomo wakati wa kutafuna kitu fulani. Hivyo, kitendo hiki husaidia sana kutunza kumbukumbu akilini mwa hadhira.

Naye mtafiti kwa upande wake pia amegundua kuwa taswira hutusaidia kutunza kumbukumbu katika nahau kwani vitu na maneno yanayorejerewa huganda sana akilini mwa msikilizaji ama msomaji. Katika mahojiano ya ana kwa ana watafitiwa wengi walisema kuwa ujumbe hupatikana kutegemea namna mtu atakavyoifafanua taswira iliyotumika kuunda neno. Watafitiwa wengi walikubaliana na mtafiti kuwa taswira zinabeba maana zaidi ya moja, na moja ya matumizi ya taswira hizi ni kutusaidia kutunza kumbukumbu ili kuweza kuitunza lugha kama kitambulisho cha jamii husika.

4.3.1.3 Taswira Itumikapo katika Neno Humjengea Hadhira Udadisi

Binadamu amejaliwa milango ya fahamu, na milango hii ndiyo humwezesha kuzindua hisia na maneno fulani katika akili yake juu ya kile anachopokea toka kwa mzungumzaji. Kutokana na hisia za kunusa, kusikia, kuona na hata kugusa. Matumizi ya taswira katika nahau huweza kuchora picha inayoibua na inayoumbwa akilini mwake baada ya kuzinduliwa na ufundi wa taswira katika matumizi ya lugha. Kwa kwaida matumizi ya taswira huweza kuhusisha kile kinachoumbwa na maisha halisi ya jamii.

Mfano katika nahau hizi;

(a) ***Kumhena*** mntu, *kumgimbika* mntu

Kiswahili: **Kumpaka mtu mafuta** kwa **mgongo wa chupa**, kumpa mtu sifa ambayo haimstahili.

Maana yake: Kumsifia mtu kwa kumpa sifa ambayo haimstahili kuwa nayo kutokana na kitendo au mambo aliyoyafanya.

Taswira inayochomoza hapa ni ya **paka mafuta** kwa **mgongo wa chupa**, mafuta yakiashiria maneno ya uongo aambiwayo mtu na mgongo wa chupa ukiashiria sifa isiyomsitahili mtu huyo kuwa nayo.

(b) *Kuja **ulala**, kuja nyemi ukibinda kuzinka mwe sungu*

Kiswahili: Kula wakati mtu amelala, kutumia kitu baada ya
kukisumbukia kwa muda mrefu.

Maana yake: Kula matunda mema baada ya kusumbukia mafanikio kwa muda mrefu.

Taswira inayojitokeza hapa ni ya **kula wakati umelala** huashiria kitendo cha mtu kustarehe baada ya kusumbukia kupata mafanikio kwa muda mrefu. Kama inavyofahamika wakati wa kutafuta mafanikio huwa ni mgumu lakini wakati mtu anapofanikiwa huwa katika starehe ya kufaidi matunda yake.

(c) ***Kumwiikaia** mntu, kumwihiwa mntu na kumuonga vibada*

Kiswahili: Kumkalia mtu kitako, kumkasirikia mtu bila sababu

Maana yake: Kumchukia mtu na kumsema maneno mabaya ambayo hayamstahili.

Taswira inayochomoza hapa ni ya **kumkalia mtu kitako** huashiria kitendo cha mtu kukaa na kuanza kuzungumza habari za mtu fulani wakati yeye hayupo. Bila shaka hili ni jambo dhahiri kuwa watu wanapohitaji kuzungumza jambo fulani kwa muda hutafuta mahali pa kuketi ili wasijichoshe kwa kitendo cha kusimama kwa muda mrefu.

(d) ***Kumng'ong'a** mntu, ni kumng'una mntu*

Kiswahili: **Kumramba mtu kisogo**, kumsema mtu maneno mabaya wakati akiwa hayupo.

Maana yake: Kumwambia mtu maneno ya kebehi.

Taswira inayochomoza hapa ni ya **kumramba mtu kisogo** huashiria kitendo cha kumnenea mtu maneno ya kebehi ya kiambatana na dharau wakati yeye mwenyewe hayupo.

(e) ***Kushisha mntu nhope**, kumuonga mntu vibada*

Kiswahili: **Paka matope**, semea mtu mabaya

Maana yake: kumchafua mtu kwa kumsema maneno mabaya, ni kuharibu sifa ya mtu kwa kumsema mabaya.

Taswira: Matope

Katika nahau hii taswira ya matope inawakilisha maneno mabaya ama jambo ambalo halistahili kumnenea mtu.

(f) ***Kumkinya mntu mhome na ndai**, kumghambia mntu mbui ye koma moyo*

Kiswahili: Kumkata mtu maini, kumwambia mtu jambo la kumkatisha tamaa

Maana yake: Habari aipatayo mtu na ikamkosesha matumaini katika kufanikisha jambo alilokuwa anatazamia mafanikio.

Taswira: maini

Katika nahau hii tunaona kuwa kitendo cha maini jinsi yanavyokatika na mara nyingi

mtu hupata maumivu makali mno, hivyo hii inaashiria kuwa mtu anaposikia habari

mbaya ya kumvunja moyo huwa anajisikia maumivu na nguvu zinamuishia.

Hivyo, idadi kubwa ya watafitiwa wameona kuwa utumiaji wa lugha katika nahau hutumia taswira kwa ajili ya kujenga udadisi kwa hadhira, mara nyingi humfikirisha

sana hadhira ili kufumbua mafumbo yaliyofumbwa ndani yake kutokana na taswira namna ilivyotumika. Matumizi mazuri ya lugha ni yale hasa yanayojenga udadisi kwa msikilizaji, taswira itumikapo huwa inafunika mambo, kusudi watu wahangaikie kufumbua na siyo kuweka wazi kila jambo. Hivyo, taswira zinazounda nahau hizi hujenga udadisi, kwani watu hujaribu kutafakari kwa kina ili kupata maudhui yake. Utumiaji wa taswira katika nahau unahitaji ubobevu wa lugha ili kuufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Taswira itumikayo ndani ya nahau ndiyo inayompatia hadhira ujumbe uliokusudiwa, kwani akishindwa kung'amua fumbo lililotumika katika lugha hawezi kupata ujumbe uliokusudiwa ndani yake. Pia, taswira itumikayo ndani ya nahau huhitaji hadhira awe mweledi wa lugha ili kuweza kuziona sitiari na tashibiha zilizotumika kuufikisha ujumbe.

4.3.2 Athari Hasi

Matumizi ya taswira katika kazi ya Fasihi simulizi hususani katika kipengele cha nahau mara nyingi huleta utata pale msikilizaji ama msomaji anaposhindwa kulielewa vema kusudio la fanani, kwani kazi ya Fasihi ni pana na kila aisomaye ama kusikia hupata dhana tofauti kulingana na uelewa wake. Vivyo hivyo, hata katika nahau za Kisambaa katika matumizi ya taswira zipo athari kadhaa zilizobainika kama zilivyoelezwa hapa chini:-

4.3.2.1 Kuleta Utata katika Matumizi yake Kulingana na Mfanano wake

Kimaana

Katika matumizi ya taswira ndani ya nahau za Kisambaa upo uwezekano wa mtu kupata mkanganyiko pale anapokutana na nahau zenye maana sawa lakini umbo na miundo yake ni tofauti. Hivyo, kuweza kuwafikirisha watumiaji wa nahau hizo na wakati mwingine kuwaletea utata hadhira katika kulitambua kusudio la fanani katika

kumfumbia hadhira fumbo alifumbue. Taswira kama kipengele cha kifani katika utanzu huu kimeonekana kuwa na uwezekano wa kuleta madhara katika ufafanuzi na uelewekaji wa nahau za Kisambaa. Mfano tunauona katika nahau zifuatazo:-

(a) *Kutoa **nenga/ holwe**, Kuvata mhombe*

Kiswahili: Kupiga **nenga**, kunywa pombe

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kitendo cha mtu kunywa pombe kupita kiasi wakati wa mapumziko.

(b) *Kutoa **mazi**, kuvata mhombe*

Kiswahili: Kupiga **maji**, kulewa pombe

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kitendo cha mtu kunywa pombe kupita kiasi.

Taswira: **Maji** yamebeba taswira ya pombe kwani vyote ni jamii za kimiminika ingawa radha ni tofauti.

(c) *Kuzwika **miwami**, kuvata mhombe*

Kiswahili: **Kuvaa miwani**, kulewa pombe

Maana yake: Kunywa pombe isivyo kawaida

Taswira: **Miwani** huashiria kitendo cha mtu aliyelewa kutokuona sawasawa na kubadili mwendo, na kutembea kama anaruka mashimo ama kupanda mlima wakati njia ipo vizuri, hivyo kufananishwa na mtu ambaye haoni sawasawa hivyo kuvaa miwani ili aweze kupata msaada wa kuona vitu.

Katika nahau (a) *kutoa nenga*, taswira tuipatayo katika nahau hii ni ya kuonekana, Taswira inayojitokeza hapa ni ya **nenga/ holwe** ambayo huashiria kinywaji aina ya pombe ya kienyeji itengenezwayo kwa miwa ambayo hutumika sana katika jamii hii ya wasambaa Ni aina ya kinywaji jamii ya kimiminika kinachotumiwa kama kiburudisho. Nahau hii inapozungumzwa katika mazingira ya kawaida mtu hawezi kuelewa kwa urahisi ni nini kusudio la mzungumzaji, lakini nahau hii ikitumika katika ufundi wa kifasihi basi hadhira huweza kufikiri ili kuweza kung'amua fumbo alilofumbiwa na fanani na kuweza kupata dhana mpya ya mtu kulewa pombe, hivyo huweza kupata maana halisi ya fumbo alilofumbiwa.

Nahau a, b na c hizi kimaana zinafanana kwa dhana ya mtu kulewa kupita kiasi pombe, hivyo matumizi yake huweza kuleta utata, kwani utata tuupatao hapa ni wa nahau tatu kuwa na maana moja ya kulewa pombe ambapo msikilizaji huweza kupata mkanganyiko katika kulielewa kusudio la fanani wake.

(a) *Kugwa tongo, n'kuhombweea*

Kiswahili: Kuangukwa na **matongotongo**, kuzubaa

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kukoua ujasiri wa kufanya jambo fulanikwa kujiamini.

Taswira: **Matongotongo** yamefananishwa na tabia ya mtu kuzubaa kwa kukosa ujasiri wa kufanya jambo kwa kujiamini.

(b) *Kutozwa n'mpheho za ng'wii, n'kuhombweea*

Kiswahili: Kushikwa na **baridi** mwilini, kuzubaa

Maana yake: Ni kukosa uchangamfu na ujasiri wa kufanya jambo fulani kwa kujiamini.

Taswira: baridi

Katika nahau hii taswira iliyojitokeza ni ya mtu kushikwa na **baridi** kunaashiria mtu kuzubaa na kukosa uchangamfu wa kufanya jambo fulani analotakiwa kufanya kwa haraka.

Nahau (a) na (b) hizi zote huashiria kitendo cha mtu kuzubaa na kukosa ujasiri wa kufanya jambo kwa kujiamini. Hivyo, hali hii huweza kuleta utata kwa hadhira pindi aambiwapo ama kuisikia nahau husika kulingana na jinji maana zake zilivyofanana na kutofautiana kimuundo tu na kimtindo pia katika muundo wake kisarufi.

(a) *Kutozeezwa ughaata, n'kuvoteka*

Kiswahili: **Kushikiwa kata**, kuomba radhi

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kujirudi / kunyenyekeana kwa kuomba radhi kwa yule uliyemkosea ama uliyemfanyia jambo ambalo halikumstahili.

Taswira: Hapa taswira tuiapatayo ni ya mtu **kushikiwa kata** ikiwakilisha kitendo cha kuomba radhi hasa kwa yule aliyemkosea mwenzake, katika jamii ya wasambaa tendo hili hufanyika wakipo mashahidi wanaowapatanisha kwa kushika kata na huambatana na maneno utakayoamriwa kunena kutoka kwa msuluhishaji.

(b) *Kuginta mazwi, kuvoteka*

Kiswahili: **Kupiga magoti**, kuomba msamaha

Maana yake: Ni tendo la kutaka radhi kwa mtu uliyemkosea katika jambo fulani

Taswira: **Kupiga magoti** huashiria kitendo cha kuomba msamaha kwa yule uliyemkosea.

Katika nahau (a) na (b) taswira inayojitokeza katika nahau hizi ni ya kuonekana, taswira ya mtu **aliyepiga magoti** na mtu **kushikiwa kata** zote zimeashiria kitendo cha mtu kuomba radhi ili kusamehewa kwa kosa alilofanya, nahau hizi zinaweza zisifahamike vizuri katika mazingira ya kawaida, lakini zikitumika katika muktadha wa kifasihi katika ufundi wa lugha hadhira huweza kufikiri kwa kina zaidi na kuweza kutoa maana halisi ya nahau hizi katika matumizi yake.

Dhana ya Umuundoleo imetusaidia sana katika kupata maana halisi zilizokusudiwa katika matumizi ya taswira ndani ya nahau za Kisambaa.

Aidha katika nahau hizi zilizotumika ni dhahiri kuwa upo utata ujitokezao katika matumizi ya nahau zinazofanana kimaana. Kwani huleta athari kubwa kwa msikilizaji, na wakati mwingine huufanya ujumbe ushindwe kueleweka kwa hadhira iliyokusudiwa pindi wanaposhindwa kuling'amua fumbo hilo kulingana na sababu hii ya kufanana kwake kimaana.

4.4 Uhusiano uliopo Baina ya Taswira Zilizomo Ndani ya Nahau za Kisambaa na Uhalisi wa Maisha ya Jamii

Ni wazi kabisa kuwa upo uhusiano mkubwa sana baina ya taswira na maneno yatumikayo kuunda nahau za Kisambaa. Maneno hayo huakisi maisha halisi ya jamii, kulingana na matendo, pamoja vitu vinavyorejelewa katika shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa ndani ya jamii hiyo, pamoja na utamaduni wake.

Uhusiano huu, huonekana pale tu nahau zinapoundwa na taswira ambayo huakisi maisha halisi ya jamii husika pamoja na kurejelea vitu vipatikanavyo katika mazingira ambapo jamii husika inaishi.

4.4.1 Huakisi Maisha Halisi katika Jamii Husika

Nahau huakisi maisha halisi ya jamii kulingana na ujumbe utolewao ndani yake, hivyo, utumiaji wa taswira hufumba jambo kwa kutumia mafumbo ya vitu vipatikanavyo ndani ya jamii husika kwa kutumia ufundi wa maneno wa hali ya juu. Maneno hayo huweza kumfikirisha hadhira kung'amua yale aliyosikia toka kwa fanani wake, hatimaye kupata kufahamu maana halisi ya neno au hata maana iliyokusudiwa na fanani wake. Vivyo hivyo, katika nahau za Kisambaa upo uhusiano wa taswira na maisha halisi ya jamii kwani huakisi yale yanayotendeka ndani ya jamii hiyo. Mfano katika nahau zifuatazo;

*(a) Kutoza **nyangio**, kuituka shita,*

Kiswahili: Kushika **mkia**, kuwa mwisho

Maana yake: Kuwa wa mwisho katika jambo ulifanyalo miongoni mwa watu.

Taswira inayopatikana hapa ni ya **mkia** ikiwa inaashiria kitu cha mwisho ambacho kimefananishwa na kiungo cha mnyama kilichoumbwa nyuma ya mnyama huyo. Hivyo, kitendo cha mtu kushika nafasi ya mwisho katika jambo hufananishwa na kiungo hicho.

*(a) Kukanda **goshi**, kushemwambiza mntu mwe kunda uambizi*

Kaswahili: Kumpa mtu **kisogo**, kuacha kumsaidia mtu

Maana yake: Ni kushindwa kutoa msaada pale mtu anapohitaji msaada kutoka kwako

Taswira chomozi ni ya **kisogo** huashiria kushindwa kutatua shida ya mtu kwa kutokuungana naye katika kulitatua tatizo lake kwa kupuuza. Kama ilivyo kawaida mtu akikugeuzia kisogo huwezi kumwona, pia ni ngumu kumweleza chochote kwasababu hutamwona mwitikio wake kama atakubali au la.

(b) ***Kumlavya mntu se mwe zua, kumuongea mntu chengoi***

Kiswahili: **Kumwanika** mtu **juani**, kusema waziwazi

Maana yake: Kuweka mambo hadharani pasipo kificho mbele ya watu kwa kumuaibisha.

Taswira inayojitokeza hapa ni ya **kuanika juani** ni ishara ya kuweka kitu wazi bila kificho yaani kitu kilicho wazi bila hata kufunikwa na huonekana na watu wote. Kadharika kitu kikiwekwa juani huonekana na kila mmoja kwani hakina kificho tena.

(c) ***Kutoighwa ntope** ya mesho, kuufigwa kwa zuuma*

Kiswahili: Kupigwa **chaga** la macho, kudanganywa wakati mtu anajua ukweli wa jambo lenyewe.

Maana yake: kudanganywa katika jambo fulani wakati ukweli unajulikana

Taswira inayochomoza hapa ni ya **changa** la macho ambalo limebeba dhana ya kudanganya, yaani udanganyifu umefananishwa na mchanga kwani uchafu huu ukimwingia mtu machoni hupata maumivu, humzuia na kumfanya mtu huyo asione

sawasawa. Hivyo, hata mtu aambiwapo habari ya uongo hushindwa kuielewa vizuri hatimaye kupata mkanganyoko juu ya habari aliyoipokea.

(d) ***Kumfuka mntu, kumwondeza mntu***

Kiswahili: **Kumchimba** mtu, ni kutafuta undani wa mtu

Maana yake: Kutaka kujua undani wa mambo ya siri ya mtu kwa kupeleleza kwa watu wengine.

Taswira: Kuchimba

(e) ***Itua mzigo, kubinda kughosha uongighwejo***

Kiswahili: Tua **mzigo**, maliza majukumu

Maana yake: Ni kumaliza kutekeleza majukumu ambayo yalikuwa yamemlema mtu kwa muda mrefu.

Taswira inayochomoza hapa ni ya **mzigo**, mzigo umewakilisha majukumu apewayo mtu kuyasimamia na kuyatekeleza. Na kitendo cha kutua huashiria kumaliza jambo na kupata pumziko.

(f) ***Kutozeezwa ughaata, n'kuvoteka***

Kiswahili: **Kushikiwa kata**, kuomba radhi

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kujirudi / kunyenyekeana kwa kuomba radhi kwa yule uliyemkosea ama uliyemfanyia jambo ambalo halikumstahili.

Taswira tuipatayo hapa ni ya mtu **kushikiwa kata** ikiwakilisha kitendo cha kuomba radhi hasa kwa yule aliyemkosea mwenzake. Katika jamii ya wasambaa tendo hili

hufanyika wakipo mashahidi wanaowapatanisha kwa kushika kata na huambatana na utamkaji wa maneno utakayoamriwa kunena kutoka kwa msuruhishaji.

(g) *Kuta **nenga**, kuvata mhombe*

Kiswahili: Kupiga **nenga**, kunywa pombe

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kunywa pombe kupita kiasi.

Taswira tuiapatayo hapa ni ya **Nenga/ holwe** ambapo huashiria kinywaji aina ya pombe ya kienyeji itengenezwayo kwa miwa ambayo hutumika sana katika jamii hii ya wasambaa. Ni aina ya kinywaji jamii ya kimiminika kinachotumiwa kama kiburudisho wakati wa mapumziko.

(h) *Kutoa **maji**, kuvata mhombe*

Kiswahili: Kupiga **maji**, kulewa pombe

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kitendo cha mtu kunywa pombe kupita kiasi.

Taswira iliyojitokeza hapa ni ya **maji** ambayo yamebeba taswira ya pombe kwani vyote ni jamii za kimiminika ingawa radha yake ni tofauti na maji katika uhalisia wake.

(i) *Kuzwika **miwani**, kuvata mhombe*

Kiswahili: kuvaa **miwani**, kulewa pombe

Maana yake: Kunywa pombe isivyo kawaida

Taswira chomozi hapa ni ya **miwani** huashiria kitendo cha mtu aliyelewa kutokuona sawasawa na kudadili mwendo, na kutembea kama anaruka mashimo ama kupanda

mlima wakati njia ipo vizuri, hivyo kufananishwa na mtu ambaye haoni sawasawa hivyo kuvaa miwani ili aweze kupata msaada wa kuona vitu.

(j) *Mashafi yana nda, fisha mbui ya sii*

Kiswahili: **Vichaka** vina **mimba**, ficha jambo la siri.

Maana yake: Tusiseme siri zetu kila mahali kwani watu wengine watasikia na kuzifikisha mahali ambapo hazikupaswa kufika.

Taswira inayopatikana hapa ni ya **vichaka** na ya **mimba**, vichaka kinaashiria mahali palipojificha na mimba inaashiria jambo la siri.

(k) *Kuja kagoghwe, kuhenya mbui*

Kiswahili: kula **gogwe**, kudanganya

Maana yake: Ni kitendo cha mtu kuongeza au kukuza jambo kwa kuongeza maneno ya uongo ndani ya habari anayopaswa kuifikisha mahali fulani.

Taswira: gogwe

Aidha, katika matumizi ya lugha, kipengele cha taswira ni moja ya kipengele ambacho kimeshika nafasi ya kipekee, kwani hutumika kwa ufundi wa hali ya juu sana kifasihi katika sanaa wa kuweza kulifumba jambo kiufundi sana hadi hadhira akashindwa kung'amua kusudi lake ndani ya tungo husika. Hivyo, upo uhusiano mkubwa sana kati ya taswira na nahau za Kisambaa katika kuyasawiri maisha halisi ya jamii husika kulingana na matumizi ya vitu vitumikavyo ambavyo hupatikana katika mazingira ya jamii ya Wasambaa na vitu hivyo humwezesha fanani kuzungumza na hadhira yake kulingana na ufundi wake wa maneno kitaswira.

4.4.2 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika sura hii tumejadili malengo haya, kuchunguza namna taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa, kuchunguza athari ya taswira katika ufafanuzi na uelewekaji wa nahau za Kisambaa kwa hadhira, kutathmini uhusiano uliopo baina ya taswira zilizomo kwenye nahau na maisha halisi ya jamii. Kwa jumla tumeona kuwa taswira zinasaidia kusawiri dunia na mambo yanayomzunguka mwanadamu, katika nahau kutokana na ukweli kuwa ni vigumu kuitenga jamii na mazingira wanamoishi. Sura hii imebainisha pia faida na hasara zinazosababishwa na matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa katika kufafanua na kuelewa ili fumbo liliofumbwa. Nahau zina matumizi makubwa ya ishara na tamathali za semi ambazo hujenga sitiari zinazotakiwa kufumbuliwa, ndipo maana ipatikane. Katika kuchunguza hili, tumeona kuwa taswira ndizo zinarahisisha shughuli za kufafanua na kuzielewa picha zilizotumika na kuziweka katika lugha ya kawaida inayoiwezesha kufumbua nahau husika. Pia, tumeweza kugundua kuwa katika mazingira anayokulia mtu yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa taswira anazopata hadhira katika nahau fulani pindi itumikapo.

SURA YA TANO

MHUTASARI, HITIMISHO, MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ametoa hitimisho la kazi hii kwa kueleza mchakato mzima uliopitiwa. Vipengele vya sura hii ni kama vifuatavyo; mhutasari wa tasnifu, ambao umesheheni yale yaliyojitokeza katika kila sura, sehemu ya pili inaeleza jinsi nadharia ilivyotumika na ilivyomsaidia mtafiti katika kuchambua na kuzijadili data zilizokusanywa. Mwisho wa sura hii ni maoni na mapendekezo.

5.2 Mhutasari wa Tasnifu

Utafiti huu umegawanyika katika sura tano, sura ambazo kila moja inafafanua vipengele maalum vya utafiti huu. Kwa ufupi sura hizi zilikuwa kama ifuatavyo: - Sura ya Kwanza, mtafiti alieleza usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti manufaa ya utafiti na jinsi nadharia ya utafiti ilivyotumika katika mchakato mzima wa kuzichambua data za utafiti.

Sura ya Pili, hapa tulifafanua mapitio ya maandiko mbalimbali ambayo yameelezea mada iliyotafitiwa. Hivyo, kutokana na mapitio hayo tumegundua yaliyojitokeza katika nahau za Kisambaa, hususani kipengele cha taswira ambacho ndio kiini cha utafiti wetu kwa kuangalia dhima ya taswira katika nahau hizo kwa jamii.

Sura ya Tatu, imezungumzia mbinu na vifaa mbalimbali vilivyotumika katika utafiti, eneo lililotumika kwenye utafiti huu pamoja na jumuiya ya watafitiwa. Vilevile sura hii imeeleza namna data za utafiti huu zilivyofafanuliwa.

Sura ya Nne, imejadili matokeo ya utafiti kwa kufafanua taswira zinavyojitokeza katika nahau kadhaa za Kisambaa. Aidha athari ya taswira katika ufafanuzi na

uelewekaji wa nahau za Kisambaa kwa hadhira pamoja na uhusiano uliopo baina ya taswira zilizomo kwenye nahau za Kisambaa na maisha halisi ya jamii umeelezwa.

Sura ya Tano na ya mwisho, imehitimisha kwa kueleza kwa ufupi jinsi kazi hii ya utafiti ilivyoweza kufikia katika ugunduzi wa yote yaliyojitokeza kulingana na kusudi la utafiti huu. Vilevile yapo mapendekezo kadhaa ya utafiti yaliyotolewa na mtafiti katika sura hii.

5.3 Utoshlevu wa Nadharia Iliyotumika katika Utafiti

Nadharia iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu ni Umuundoleo kutokana na msingi mkuu wa nadharia hiyo, ambayo inachukua nafasi kubwa katika kuchanganua muundo wa jamii wa maana pamoja na uwezo wa ung'amuzi kibinafsi, katika mawanda ya kifasihi. Umuundoleo unaangalia lugha kama nguzo ambapo maana halisi au inayowezekana pamoja na matokeo yake huelezwa. Hivyo, nadharia hii ilitumika katika kutambua namna taswira zinavyojitokeza katika nahau za Kisambaa, athari ya matumizi ya taswira katika uelewekaji na ufafanuzi wa nahau za kisambaa kwa hadhira, pamoja na uhusiano uliopo baina ya taswira zilizomo katika nahau za Kisambaa na maisha halisi ya jamii.

5.4 Mchango Mpya wa Utafiti Huu

Utafiti huu umedhihirisha kuwa yapo maneno ya Kisambaa ambayo yalitumika zamani na hayatumiki sana katika nyakati za leo. Hivyo, sehemu kubwa ya kizazi cha wasambaa wa sasa wanayaona maneno hayo kuwa ni mapya katika matumizi yake ndani ya lugha yao. Mfano wa maneno hayo ni kama *kaoka*, *kighija*, *mngoi*, *uzumbe*, *gutwi*, *sakame*, *chengoi*, *ughaata*, *mbila* na *mbughe*. Vilevile jambo hili kuonekana kuwa linaweza kuathiri sehemu kubwa katika lugha hii ya Kisambaa kwa kupotea kabisa kwa maneno hayo kutokana na kukosa watumiaji wake, kwani lugha

ikikosa watumiaji hupotea na mwishowe hufa kabisa. Hivyo, hata maneno hayo ya Kisambaa yakikosa watumiaji katika jamii ya wasambaa ipo hatari ya kupotea na kuleteleza lugha hiyo kutumia maneno mengi ya kisasa kwa kuyatohoa kutoka lugha ya Kiswahili na mwishowe kupoteza thamani na radha yake kabisa.

Jambo jingine jipya ni kule kufanana kwa maana katika baadhi ya nahau za Kisambaa lakini zikiwa na maumbo na muundo tofauti kisarufi. Zipo nahau za Kisambaa ambazo zimegundulika kuwa na sifa hiyo, nahau hizi wakati mwingine kuleta utata kwa hadhira katika kuling'amua kusudio la fanani.

Jambo jingine lililoibuliwa na utafiti huu, ni kuwepo kwa maneno mbalimbali ya lugha ya Kisambaa ambayo yanafanana na yale ya Kiswahili. Hivyo kuwepo kwa tofauti za kisarufi tu ndani yake, mfano katika nahau kadhaa za Kisambaa zilizoonesha ukaribu wa maneno hayo ni hizi zifuatazo,

Kisambaa	Kiswahili
Mesho	macho
Shikio	sikio
Kabui	kaburi
Goghwe	gogwe
Zisho	jicho
Kuja	kula

Jambo jingine jipya lililojitokeza ni kwamba sio maneno yote ya Kisambaa ambayo tunaweza kupata mbadala wake katika lugha ya Kiswahili, hivyo kuweza kuyatumia kama yalivyo kwa kuyatolea ufafanuzi wake ili kuweza kufahamika kwa hadhira ambao hawaifahamu lugha hiyo. Mfano maneno kama *uzozo*, *kaoka*, *nenga* na *holwe*.

Hata hivyo, taasisi ya elimu kupitia Idara ya Fasihi ya Kiswahili wawe na jukumu la kuimarisha kazi mbalimbali za Fasihi, ambazo zipo kwenye hatari ya kupotea hususani zilizopo katika lugha za kikabila. Wanafunzi wawe na tabia ya kupenda kufanya tafiti katika jamii zao za asili, kwa kukusanya Fasihi simulizi kama sehemu ya mafunzo ya taaluma zao ili kuimarisha lugha hizo. Pia ni muhimu wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari wawe na tabia ya kwenda kujifunza asili ya lugha zao vijijini kwao pindi wawapo likizo ili kujiimarisha katika lugha hizo na kujua asili ya jami zao.

Vilevile kuwepo na kamusi zilizoandaliwa kwa lugha ya asili ili kuweza kuimarisha na kuzihifadhi lugha, hii itasaidia watu wengine kujifunza zaidi kupitia kamusi hizo.

Ni vema kuwepo na maktaba katika maeneo ya utafiti kusudi jamii zilizotafitiwa waweze kuyafaidi matokeo ya utafiti uliofanyika katika maeneo yao, kwani matokeo ya utafiti yakijulikana kwa watoa data yatasaidia kuinua ufahamu wao juu ya mambo yanayowahusu.

5.5 Mapendekezo Juu ya Tafiti Zijazo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu ni wazi kuwa fani, hasa kipengele cha matumizi ya lugha katika Fasihi simulizi hakijafanyiwa tafiti za kutosha kama ilivyo katika maudhui ya nahau ambavyo yameshughulikiwa kwa mapana. Hivyo, watafiti mbalimbali wanapaswa waendeleze tafiti zao juu ya vipengele vingine vilivyomo katika matumizi ya lugha kama vile kipengele cha tamathali za semi katika lugha zao za asili.

MAREJELEO

- Balisidya, M. L. (1987), "Tanzu na Fasihi za Fasihi Simulizi", *Mulika* Na.19.uk.2-9. TUKI. Dar es Salaam
- Douglu Biber, na wenzake (2002) *The Longman Student Grammar of Spoken and Written English*. Northern Arizona University
- Kahigi, K. K na Mulokozi, M.M (1982) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam
- Kamusi ya Kiswahili karne ya 21 (2011) Longhorn Publisher, Nairobi
- Kimani Njogu & Richard M. Wafula (2007), *Nadharia za Uihakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Sai Industries ltd, Nairobi
- Kombo, K. D na Tromp, D.L.A (2006) *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*, Pulines Publisher, Nairobi
- Kothari, C. R. (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*. 2nd Revised Edt. New Age International Publishers Ltd, New Delhi
- Kuhenga, C. (1980), *Nahau za Kiswahil: Jendwali la Misemo ya Lugha*. Arusha, Tanzania: Eastern Afrca Publications
- Madumulla, J. S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Mture Education Publishers. LTD, Dar-es Salaam
- Madumulla, J. S. (1995), *Proverbs and Sayngs: Theory and Practice*, Dar es Salaam, University of Dar es salaam
- Masunga S. T (2012) "Taswira na ishara katika ushairi wa Mathias E. Mnyampala" Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)
- Mauya, A. B.S (2006), *Semi: Maana na Matumizi*, TUKI, Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M (1989), *Tanzu za Fasihi simulizi*, Mulika Na. 21: 1-24 TUKI. Da es Salaam
- (1990), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam

- (2003), *Utafiti wa Fasihi Simulizi. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. TUKI. Dar es Salaam
- Mrekwa A. S (2013) “Taswira katika Ushairi wa Kaluta Amri Abedi” Tasnifu kwa Ajili ya Kukamilisha Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)
- Njogu, K & Chimerah, R (1999), *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Nyenye M. A (2011) “Taswira zinazojitokeza katika Nathari za Euprase Kezilahabi: Nagona na Mzingire Tasnifu kwa Ajili ya Kukamilisha Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa)
- Senkoro, F.E.M.K (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: Press Publicity Center
- (2011), *Fasihi*, KAUTTO, Limited. Dar es Salaam
- Shulman, R (1988), *Contemporary Methods for Resesarch Education*. American Education Resesarch Association, Washington DC.
- TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili*. TUKI. Dar es Salaam
- Wamitila, K, W (2003), *Kichocheo cha Fasihi Simuluzi Andishi*. Nairobi, Kenya: Focus Publications.
- (2004), *Kichocheo cha Fasihi Simuizi na Andishi*. Nairobi Focus Publisher. LTD
- (2008), *Kanzi ya Fasihi . Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Vide-Muwa Publisher. LTD
- Wanjala F. Simiyu (2011), *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa shule Ndaki na Vyuo*. Dares Salaam: Press Publicity Center.

VIAMBATISHO

A.1 Mwongozo wa Mahojiano kwa Wazee (ambao sio wasomi)

Muongozo wa maswali ya utafiti kwa wazawa wa kabila la Wasambaa ambao hawapo katika kundi la wasomi.

TAARIFA ZA MTAFITI

Mtafiti ni mwanachuo wa chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) wa ngazi ya uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (MA KISWAHLI LITERATURE). Utafiti huu unahusu dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa. Unaombwa kutoa mchango wako kadiri uwezavyo na unahakikishiwa kuwa maelezo utakayoyatoa yatatumiwa kwa kuleta ufanisi kwa malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

SEHEMU YA KWANZA

TAARIFA ZA MTAFITIWA

Jaza kwa kuweka alama ya vema katika nafasi iliyoachwa wazi au kwa kujaza maelezo mafupi.

Jina (si lazima).....

Jinsia: MKE, MME.....

Umri.....

Unapoishi.....

SEHEMU YA PILI

Maswali ya watafitiwa

1/. je kuna tofauti ya lugha ambazo mlikuwa mnazitumia zamani na lugha ambazo mnazitumia sasa hivi?

2/ kama zipo ni zipi tofauti hizo?

3/ Je katika mazungumzo yenu ya kawaida katika kuwaasa vijana mlikuwa mnatumia lugha za wazi au za mafumbo?

Lugha za waziMafumbo.....

4/. Kama ni lugha za mafumbo mlizokuwa mnatumia ni mafumbo ya namna gani? methali, nahau, vitendawili na misemo.

5/. Ni athari gani zilikuwa zinazojitokeza katika matumizi ya lugha hizo kwa jamii?

6/. Toa maoni yako kwa jumla juu ya dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa.

7/. (a) Moja kati ya lugha za mambo yaliyotajwa hapo juu zikiwemo methali, nahau, vitendawili na misemo ndizo zinazounda lugha ya mafumbo, wewe unafahamu nini kuhusu nahau?

(b). Naomba unitajie nahau kumi za Kisambaa zinazofanana na hizi;

i/ Mtu wa miraba minne

.....

ii/ Amekula chunvi nyingi

.....

iii/ amekuwa popo

.....

iv/ paka mafuta kwa mgongo wa chupa

.....

v/ Ana mkono wa birika

.....

vi/ kumvika mtu kilemba cha ukoka

.....

vii/ kumpa (mtu) nyama ya ulimi

.....

viii/. Kumwonyesha mtu mgongo

.....

ix/. Hawapikiki katika chungu kimoja

.....

x/. Kuvunja ungo

.....

8/. Taja nahau kumi za Kisambaa unazozifahamu tofauti na hizo ulizotaja hapo juu.

A.2 Muongozo wa Mahojiano kwa Wazee (ambao niwasomi)

Muongozo wa maswali ya utafiti kwa wazawa wa kabila la Wasambaa ambao wapo katika kundi la wasomi.

TAARIFA ZA MTAFITI

Mtafiti na mwanachuo wa chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) wa ngazi ya uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (MA KISWAHLI LITERATURE). Utafiti huu unahusu dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa. Unaombwa kutoa mchango wako kadiri uwezavyo na unahakikishiwa kuwa maelezo utakayoyatoa yatatumiwa kwa kuleta ufanisi kwa malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

SEHEMU YA KWANZA

TAARIFA ZA MTAFITIWA

Jaza kwa kuweka alama ya vema katika nafasi iliyoachwa wazi au kwa kujaza maelezo mafupi.

Jina (si lazima).....

Jinsia: MKE, MME.....

Umri.....

Unapoishi.....

Kiwanga cha Elimu; Elimu ya Sekondari, Stashahanda, Shahada ya Chuo kikuu.....

SEHEMU YA PILI

1/. (A) Eleza maana ya nahau jinsi unavyoifahamu

(B) Taja nahau kumi za Kisambaa unazozifahamu

2. Andika nahau zifuatazo kwa lugha ya Kisambaa kisha eleze funzo litolewalo kwa jamii kupitia nahau hizo.

i /. Kumwuma mtu sikio

.....

ii /. Kukunja uso

.....

iii /. Kupiga chuku

.....

iv /. Paka mafuta kwa mgongo wa chupa

.....

v /. Amenitoka machoni

.....

3/Taswira zina athari zipi katika kuelewa nahau

Taja athari chanya na hasi zinatokana na matumizi ya taswira katika nahau.

4/. Toa maoni yako kwa jumla juu ya dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa

5/. Ni taswira, picha, ishara, mafumbo yepi yanayojitokeza katika nahau hizo na zina maana gani?

6/. Ni sababu ipi / zipi zilizofanya kutumia taswira?

7/. Je, taswira zina umuhimu gani katika nahau za Kisambaa?

8/. Je, matumizi ya taswira, picha, mafumbo katika nahau za Kisambaa zina athari gani kwa hadhira?

9/. Toa maoni yako juu ya matumizi ya lugha ya picha, taswira, mafumbo katika nahau za Kisambaa.

10/. Matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa yana nafasi gani katika wakati wa sasa.

A.3 Mwongozo wa Dodoso kwa Wanachuo

Muongozo wa dodoso ya maswali ya utafiti kwa wanachuo wa Sebastian Kolowa (SEKOMU) wanaosoma Fasihi ya Kiswahili.

TAARIFA ZA MTAFITI

Mtafiti ni mwanachuo wa chuo kikuu cha Dodoma wa ngazi ya uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (MA KISWAHLI LITERATURE). Utafiti huu unahusu dhima ya taswira katika nahau za Kisambaa. Unaombwa kutoa mchango wako kadiri uwezavyo na unahakikishiwa kuwa maelezo utakayoyatoa yatatumiwa kwa kuleta ufanisi kwa malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

SEHEMU A

TAARIFA ZA MTAFITIWA

Jaza kwa kuweka alama ya vema katika nafasi iliyoachwa wazi au kwa kujaza maelezo mafupi.

Jina (si lazima).....

Jinsia: MKE, MME.....

Umri.....

Unapoishi.....

Kiwanga cha Elimu; Elimu ya Sekondari, Stashahanda, Shahada ya Chuo kikuu.....

1 /. Nahau hutumia lugha ya namna gani?

2 /. Unafikiri lugha hiyo hutumika kwa madhumuni gani?

3 /. Kwa nini nahau hutumia maneno machache kuliko methali au mafumbo?

4 /. Semi ni moja ya tanzu za Fasihi simulizi ambayo hutumia lugha ambayo haipo wazi, Je unafikiri lugha hiyo ni mafumbo, methali ama nahau?

5/. Nahau zenye kutumia taswira zina athari namna kwa namna kwa jamii.

Kama unaunga mkono taja athari tatu, chanya na hasi kama zipo zinazotokana na matumizi ya taswira katika nahau.

7/. Toa maoni yako kwa jumla juu ya Dhima ya taswira katika nahau.

8/. Ni taswira, picha, ishara, mafumbo yepi yanayojitokeza katika nahau hizo na zina maana gani?

9/. Ni sababu ipi / zipi zilizofanya kutumia taswira?

10/. Je, matumizi ya taswira, picha, mafumbo katika nahau zina athari gani kwa hadhira.

11/. Toa maoni yako juu ya matumizi ya lugha ya picha, taswira, mafumbo katika nahau.

12/. Matumizi ya taswira katika nahau yana nafasi gani katika wakati wa sasa.

13/.Eleza uhusiano uliopo kati ya taswira zilizomo kwenye nahau na maisha halisi ya jamii?

B. Orodha ya Nahau ya Kisambaa Zilizotumika katika Utafiti Huu

1. Mashafi yana nda, fisha mbui ya sii

Kiswahili: Vichaka vina mimba, ficha jambo la siri

2. Kukong'wa n'zisho jako, kushaghua kihnu kibada

Kiswahili: kuponzwa na jicho lako, fanya uamuzi usio sahihi.

3. Kuja kagoghwe, kuhenya mbui

Kiswahili: Kula gogwe, kudanganya

4. Kughoshoa ndima ya gunda, ndima ishinayo maiho

Kiswahili: Kufanya kazi ya msaragambo, kazi isiyo na tija

5. Kuja kaoka, kuja sungu nyingi mwe ndima

Kiswahili: kula kitu kilichochoywa, kupata shida na adha

6. Mntu mbughe, mntu mwena choyo.

Kiswahili: mtu mbughe, mtu mchoyo

7. Kuita uzozo, kutozeezwa viugho

Kiswahili: kutekwa ufahamu/ akili kupumbazwa akili kwa soga za wengine

8. Kutana na ubweni, n'kughua mvyee

Kiswahili: kuachana na ukapera, kupata jiko, kuoia mke

9. Kutoza funda, n'kutozwa n'fanyanyi

Kiswahili: Kushika shavu, kuhuzunika

10. Gea utambi, kushongeeza mbui

Kiswahili: Tia utambi, chochea jambo

11. Kuvutika mtwi, n'kugimbikwa

Kiswahili: Vimba kichwa, pata sifa

12. Kumja mntu gutwi, kumghambia mbui ya sii

Kiswahili: Kumng'ata mtu sikio, kumnong'oneza jambo

13. Haka mikono, kukiavya mwe mbui

Kiswahili: nawa mikono, kujikoa

14. Azatoza uzumbe, kuwaongoza wantu

Kiswahili: shika usukani, kuongoza

15. Ulimi wa uona, kuongoza mbui ya mambeza ushieneyo

Kiswahili: kusema maneno ya uongo sema jambo ambalo hujalishuhudia kwa macho

16. Kushungia kabui/ tubwi, n'kuhuma kuhuma hehi na kufa

Kiswahili: Kuchungulia kaburi, mtu kuugua hata kukaribia kufa

17. Kumhena mntu, kumgimbika mntu

Kiswahili: Kumpaka mtu mafuta kwa mgongo wa chupa, kumpa mtu sifa ambayo haimstahili.

18. Kuja ulala, kuja nyemi ukibinda kuzimha mwe ndima

Kiswahili: Kula wakati mtu amelala, kutumia kitu badala ya kukisumbukia kwa muda mrefu.

19. Kumwiikaia mntu, n'kumng'una mntu

Kiswahili: Kumramba mtu kisogo, kumsema mtu maneno mabaya wakati akiwa hayupo

20. Kutoa nenga/ holwe, kuvata mhombe

Kiswahili: kupiga nenga, kunywa pombe

21. Kutoa mazi, kuvata mhombe

Kiswahili: kupiga maji, kulewa pombe

22. Kuzwika miwani, kuvata mhombe

Kiswahili: kuvaa miwani, kulewa pombe

23. Kugwa tongo, n'kuhombweea

Kiswahili: Kuangukwa na matongotongo, kuzubaa

24. Kutozwa n'mpeho za ng'wii, n'kuhombweea

Kiswahili: kushikwa na baridi mwilini, kuzubaa

26. Kutozeezwa ughaata, n'kuvuteka

Kiswahili: kushikiwa kata, kuomba radhi

27. Kuginha mazwi, n'kuvoteka

Kiswahili: Kupiga magoti, Kuomba msamaha

28. Kutoza nyangio, kuituka shita

Kiswahili: Kushika mkia, kuwa wa mwisho

29. Kukanda goshi, kushemwambiza mntu mwekunda uambizi

Kiswahili: Kumpa mtu kisogo, acha kumsaidia mtu

30. Kumlavya mntu se mwe zua, kumuongea mntu chengoi

Kiswahili: Kumwanika mtu juani, kusema waziwazi

31. Kutoighwa nhope ya mesho, kuufighwa kwa zuuma

Kiswahili: Kupigwa change la macho, kudanganywa wakati mtu anajua ukweli wa jambo lenyewe

32. Kumfuka mntu, n'kumwandeza mntu

Kiswahili: Kumchimba mtu, kutafuta undani wa mtu

33. Itua mzigo, kubinda kughosha uongiwejo

Kiswahili: Tua mzigo, maliza majukumu

34. Kushisha mntu nhope, kumuonga mntu vibada

Kiswahili: Paka matope, semea mtu mabaya

35. Kumkinya mntu mhome na ndai, kumghambia mntu mbui ye koma moyo

Kiswahili: Kumkata mtu maini, kumwambia mtu jambo la kumkatisha tamaa

C: Picha Mbalimbali Kuhusiana na Utafiti



Picha namba 1: Mtafiti (aliyevaa sweta jeupe) akiwa na wanachuo wa shahada ya kwanza ya Fasihi simulizi wakiwa katika mjadala wa vikundi. (Utafiti, Juni, 2015)



Picha namba 2: Mtafiti (upande wa kulia) akiwa katika vikundi vya watafitiwa na kutoa msaaada kwa watafitiwa pale inapobidi, (Utafiti, Juni, 2015)



Picha namba 3: Mtafiti (upande wa kulia) akiwa na watafitiwa katika kujadili uhusiano uliopo kati ya matumizi taswira katika nahau za Kisambaa na maisha halisi katika jamii, (Utafiti, Juni, 2015)



Picha namba 4: Mtafiti (upande wa kushoto) akiwa na watafitiwa wakitoa michango yao kuhusu athari zinazojitokeza katika matumizi ya taswira katika nahau za Kisambaa (Utafiti, Juni 2015)



Picha namba 5: Mtafiti akiwa katikati akinukuu michango ya wazee kuhusu athari wazipatazo ndani ya nahau katika nahau za Kisambaa, (Utafiti, Juni, 2015)